Fahari Yetu:
Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Na

Dosteus M. Lopa

Antipacy Shinyambala

Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Dar es Salaam, Tanzania, Machi, 2025

Dibaji

Ndugu msomaji, ndugu yetu katika Kristo, na Mwenyekiti wa Kanda ya Mt. Marko, Dosteus Lopa, akimshirikisha Ndugu Antipacy Shinyambala wamejitolea kutuandikia kitabu kuhusu historia ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe tangu ilivyoanza kama kituo cha sala mpaka ilivyo sasa mwaka huu 2025. Historia ya Parokia hii ya Bikira Maria Consolata Makabe ni muhimu kwa Kanisa letu la Makabe na makanisa mengine ya Jimbo Kuu la Dar es Salaam na majimbo mengine kwani limepata maendeleo ya haraka sana kwa muda mfupi. Historia hii ya Parokia ya Makabe ni muhimu kwa kuwa waandishi wameainisha mipango na mbinu mbalimbali zilizotumika kuijenga Parokia ya Makabe. Njia hizo ni pamoja na namna waamini walivyojitoa kulijenga Kanisa lao kwa njia ya Sadaka, Zaka na Tegemeza Parokia na michango kwa ajili ya ujenzi ambayo hugawanywa kwenye Kanda na Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK).

Zaidi ya hayo ndugu msomaji, Ndugu zetu hawa Lopa na Shinyambala wametusaidia kuweka kwenye kumbukumbu isiyofutika kwa ajili ya kizazi chetu na vizazi vijavyo watu waliowahi kujitolea kwa namna tofauti katika kuiongoza Parokia ya Makabe. Nawapongeza kwa hili kwani bila juhudi zao za pamoja majina ya Mapadre, Makatekista na Viongozi Walei waliowahi kutumika kwenye kazi ya Bwana Parokiani Makabe wasingejulikana kama walishaifanya kazi ya Bwana katika Parokia hii ya Bikira Maria Consolata Makabe. Pamoja na watu waliotumikia Parokia ya Makabe yapo matukio mbalimbali ambayo kwa hali ya kawaida tusingekuwa na kumbukumbu ya lini yalifanyika. Kitabu hiki kiwe msaada kwa Mapadre, Makatekista na Walei wote kuhusu watu na matukio yaliyopangwa na kufanyika katika Parokia yetu pendwa ya Makabe.

Fahari Yetu ni kitabu kinachotupatia 'uhondo' huo wote ambao wewe ndugu msomaji utakufanya ujisikie fahari kuwa mwanaparokia wa Makabe au kujua makubwa haya ya Mungu waliyofanya Wanamakabe kwa sifa na utukufu wa Mungu. Hivyo ndugu msomaji karibu ushiriki fahari hiyo kwa kuijua Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe na ujifunze matukio yote yaliyofanywa na Parokia yetu pendwa tangu kilipokuwa Kituo cha Sala, Kigango, na Parokia ambayo ikawa na vigango 3 ambavyo ikavilea hadi kuwa Parokia zinazojitegemea. Ni imani yangu kuwa utafurahia kitabu hiki na kuungana na Wanaparokia ya Makabe kumshukuru Mungu kwa safari ya kuijenga Parokia ambayo pasipo shaka waliongozwa na bado wanaongozwa na ***Zaburi ya 127: 1: Bwana asipoijenga nyumba Waijengao wanafanya kazi bure. Bwana asipoulinda mji, Yeye aulindaye akesha bure.*** Hii ikiwa na tafsiri fupi tu kwamba waamini wa Parokia ya Makabe wamelindwa na Mungu katika ujenzi wa Parokia yao ambayo kwa muda mfupi imekuwa moja ya Parokia maarufu na inayotegemewa ya Jimbo Kuu la Dares Salaam.

Nakutakia usomaji mwema

Dkt. Innocent Kangalawe
Mjumbe wa HWP kupitia Jumuiya Ndogo Ndogo ya Kikristo ya Mt. Monica,
Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe, Jimbo Kuu la Dar es Salaam

Yaliyomo

Dibaji i

Majedwali yaliyomo x

Picha zilizomo xi

Orodha ya vifupisho xii

Salamu za Baba Paroko wa Parokia ya Bikira Maria Consolata - Makabe xiii

Pongezi na Shukurani xvii

SURA YA KWANZA 1

Utangulizi 1

Maelezo ya Usuli 1

Mahali ilipo Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 3

Mandhari 5

Huduma za kijamii na kiuchumi 5

SURA YA PILI 8

Historia ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 8

Safari ya kuwa Parokia 8

Kituo cha Sala Makabe 8

Kupanda hadhi na kuwa Kigango cha Makabe 10

Kupanda Hadhi na kuwa Parokia ya Makabe 11

Vigango vya Parokia ya Makabe 13

Miaka 15 sasa (Machi 2024) tangu kuwa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 15

Huduma za Kichungaji Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 16

Huduma zingine za kiroho na kichungaji 19

Masista wa Kwanza Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 21

Parokia ya Ubungo-Msewe chimbuko la Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 25

SURA YA TATU 27

Harakati Mithilika za Maendeleo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 27

Uongozi na Harakati za Kufanikisha Maendeleo 27

Uongozi wakati Makabe bado Kituo cha Sala 27

Uongozi wakati ikiwa Kigango cha Makabe 28

Wanamakabe kuwa ndani ya Uongozi wa Juu wa Parokia 29

Uongozi baada ya kuwa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 32

Ushiriki wa Viongozi Wakuu wa Kanisa katika maendeleo ya Parokia 38

Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam 38

Marafiki Mapadre na Wengine wa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 54

Makatekista: Nguzo Muhimu Ya Parokia Ya Makabe 64

Orodha ya Makatekista wa Parokia ya Makabe 66

Mikakati na Michakato ya kufanikisha maendeleo 67

Ushiriki wa Vyama vya Kitume vya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 67

Ushirikishwaji wa Wanaparokia wa Parokia ya Makabe 69

SURA YA NNE 77

Maendeleo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 77

Ujenzi wa Kanisa la kwanza, Nyumba ya Mapadre na Ofisi za kwanza za Parokia 77

Ujenzi wa Kanisa Kubwa la Kudumu 79

Ujenzi wa Ofisi Nzuri za Parokia 82

Mandhari na Mazingira ya Parokia ya Makabe 82

Maendeleo ya huduma za Imani katika Parokia Bikira Maria Consolata Makabe 83

Kuongeza maeneo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe 86

Uwezo wa Parokia kujitegemea 88

Maendeleo ya huduma za kijamii na kiuchumi **Error! Bookmark not defined.**

Bahati za kipekee za Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo kazindua Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe ni Parokia ya Kwanza ya Utumishi wa Shirika la MMI **Error! Bookmark not defined.**

Kanisa la Kwanza Kutabarukiwa na Mhashamu Askofu Mkuu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi kama Mkuu wa Jimbo **Error! Bookmark not defined.**

Parokia ya tatu kwa Askofu Henry Mchamungu kutoa Sakramenti ya Kipaimara tangu apewe Daraja Takatifu la Uaskofu **Error! Bookmark not defined.**

Parokia ya kwanza kuagizwa na kutekeleza ujenzi wa jengo moja lenye Kanisa la kuabudia, Groto la Mama Bikira Maria na la Mtakaktifu Yosefu **Error! Bookmark not defined.**

Mkutano wa Hamlashauri ya Walei Jimbo Kufanyika Parokiani Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Parokia ya mwisho Askofu Stephano Lameck Musomba (OSA) kuadhimisha Ibada ya Misa ya Jumatano ya Majivu akiwa Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam **Error! Bookmark not defined.**

Utamaduni wa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Mila na desturi ya kutoa salamu maalumu wakati wa sikukuu za Kanisa **Error! Bookmark not defined.**

Utamadumi wa risala kwa viongozi wa Kanisa **Error! Bookmark not defined.**

Maadhimisho ya Somo wa Parokia ni sherehe ya kujumuika Parokiani kwa kusali, kushangilia, kula na kunywa pamoja **Error! Bookmark not defined.**

Kuvaa sare ya Parokia wakati wa matukio yote makubwa ya Kanisa ndani na nje ya Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Ukarimu na zawadi kwa Maaskofu **Error! Bookmark not defined.**

Utoaji zawadi wakati wa sikukuu za Kanisa **Error! Bookmark not defined.**

Kutoa machapisho ikiwamo vitabu ili kuwapa taarifa Wanaparokia na Kanisa kwa ujumla **Error! Bookmark not defined.**

Kuandaa kampeni mbalimbali kwa mfumo wa mashindano **Error! Bookmark not defined.**

Parokia zilizozaliwa kutoka Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Parokia ya Mt. Theresia Benedicto wa Msalaba Msumi **Error! Bookmark not defined.**

Parokia ya Bikira Maria Immaculata Pande **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TANO **Error! Bookmark not defined.**

Matoleo na Kuitegemeza Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe**Error! Bookm**

Zaka **Error! Bookmark not defined.**

Utoaji wa Zaka Katika Parokia ya Makabe: Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa **Error! Bookmark not defined.**

Hali ya Utoaji wa Zaka na Changamoto Zilizopo **Error! Bookmark not defined.**

Hatua Zilizochukuliwa Kuboresha Utoaji wa Zaka **Error! Bookmark not defined.**

Tathmini ya hali ya Utoaji Zaka **Error! Bookmark not defined.**

Mifumo Rasmi ya Utoaji Zaka Kidijiti **Error! Bookmark not defined.**

Mavuno ya Parokia na Jimbo **Error! Bookmark not defined.**

Sadaka: Msingi wa Ibada na Maendeleo ya Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Matoleo Binafsi ya Hali na Mali: Ustawi wa Parokia ya Makabe **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SITA **Error! Bookmark not defined.**

Miaka 10 ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe **Error! Bookmark not defi**

Maadhimisho ya Miaka 10 ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Uzinduzi wa Madhimisho ya Miaka 10 ya Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Kutabaruku Kanisa na Altare **Error! Bookmark not defined.**

Maandalizi ya Sherehe **Error! Bookmark not defined.**

Matukio mbalimbali ya Maadhimisho ya Miaka 10 ya Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 10 ya Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Matokeo ya Maadhimisho ya Miaka 10 ya Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Mwamko Mpya na Kuongeza Idadi ya Misa Takatifu **Error! Bookmark not defined.**

Sherehe za Somo wa Parokia ya Makabe **Error! Bookmark not defined.**

Mabadiliko ya Siku ya Maadhimisho ya Somo wa Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Madarasa na Misa Takatifu ya Watoto siku za Jumapili **Error! Bookmark not defined.**

Ushiriki wa watoto katika Misa Takatifu na Ibada mbalimbali **Error! Bookmark not defined.**

Usalama wa Watoto Kanisani **Error! Bookmark not defined.**

Uhamasishaji wa Misa ya Watoto **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SABA **Error! Bookmark not defined.**

Maendeleo Mapya ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe**Error! Bookmark**

Ujenzi wa Kanisa la Kuabudia na Groto la Mama Bikira Maria na la Mt. Yosefu **Error! Bookmark not defined.**

Wazo na mpango wa kuwa na Kanisa la Kuabudia na Groto **Error! Bookmark not defined.**

Safari ya Ujenzi kwa Imani, Moyo Mmoja na Ushirikiano **Error! Bookmark not defined.**

Kubariki na Kuzindua Kanisa la Kuabudia **Error! Bookmark not defined.**

Usanifu na Mandhari ya Kanisa la kuabudia na Grotto la Mama Bikira Maria na la Mtakatifu Yosefu **Error! Bookmark not defined.**

Matumizi mazuri ya Kanisa la Kuabudia na Magroto hayo **Error! Bookmark not defined.**

Darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Chimbuko la wazo la darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Mchakato wa utekelezaji wa wazo la darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Uendeshaji wa darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Njia au Mbinu zinazotumika katika darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Matokeo yanayopatikana kwa kuendesha darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Ushauri na mawazo ya kuboresha darasa la Biblia **Error! Bookmark not defined.**

Ununuzi ya Gari Jipya la Parokia **Error! Bookmark not defined.**

Ujenzi wa Nyumba Mpya ya Mapadre **Error! Bookmark not defined.**

Majedwali yaliyomo

Jedwali la 1: Maparoko, Maparoko Wasaidizi, Masista na Makatekista kati ya 2010 hadi 2022
Jedwali la 2: Parokia zilizosimamia Kigango cha Makabe kabla ya kuwa Parokia kamili
Jedwali la 3: Parokia zilizokuwa Vigango vya Parokia ya Makabe yaani Msumi, Tegeta 'A' na Pande
Jedwali la 4: Viongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia (HWP) tangu kuanzishwa kwa Parokia
Jadwali la 5: Vyama vya Kitume katika kushiriki maendeleo Parokiani Makabe
Jadwali la 6: Baadhi ya Kamati za kuratibu na kusimamia maendeleo Parokiani Makabe
Jadwali la 7: Sakramenti Takatifu zilizotolewa wakati wa Maadhimisho ya miaka 10 ya Parokia
Jadwali la 8: Kwaya zilizoshiriki Tamasha la Kwaya katika Maadhimisho ya miaka 10 ya Parokia

Picha zilizomo

Picha ya1: Kanisa la kwanza la Parokia Makabe lililojengwa miaka ya mwanzo ya 1980

Orodha ya vifupisho

1.	BMC	-	Bikira Maria Consolata
2.	I.M.C[1]	-	Wamisionari wa Bikira Maria Consolata
3.	CPT	-	Christian Profeional in Tanzania
4.	Dkt	-	Daktari wa Salfasa
5.	HWP	-	Halmasshauri ya Walei Parokia
6.	JNNK	-	Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo
7.	KTP	-	Kamati Tendaji Parokia
8.	Mat.	-	Matendo ya Mitume
9.	Mha.	-	Mhashamu
10.	Mh.	-	Mheshimiwa
11.	MMI[2]	-	Shirika la Wamisionari wa Maria Imakulata
12.	Mt.	-	Mtakatifu
13.	Mwl.	-	Mwalimu
14.	Ndg.	-	Ndugu
15.	Pd.	-	Padre
16.	SACCOS[3]	-	Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo
17.	Sr[4].	-	Sista
18.	UWAKA	-	Utume wa Wanaume Katoliki
19.	VIWAWA	-	Vijana Wakatoliki Wafanyakazi
20.	WAWATA	-	Wanawake Wakatoliki Tanzania

[1]Kwa Kiingereza I.M.C ni Consolata Missioneries
[2]Kwa Kiingereza MMI ni Missionaries of Mary Immaculate
[3] Kwa kiingereza SACCOS ni Savings and Credit Co-Operative Society
[4] Kwa Kiingereza Sr. ni Sister

Salamu za Baba Paroko wa Parokia ya Bikira Maria Consolata - Makabe

Ndugu wapendwa katika Kristo,

Tumsifu Yesu Kristo!

Kwa furaha kubwa na shukrani za dhati, nawasalimia ninyi Wanaparokia wa Makabe katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Napenda kuwapongeza kwa namna mnavyoendelea kushiriki kwa moyo mmoja katika safari hii takatifu ya kumtumikia Mungu kwa imani, upendo, na mshikamano wa kweli.

Ninaendelea kumshukuru Mungu kwa ajili yenu, kwa sababu ya upendo, imani, na moyo wa kujitoa mnaouonesha kila siku kwa ajili ya ustawi wa Parokia yetu pendwa ya Bikira Maria Consolata Makabe. Ushirikiano wenu katika Ibada, Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK), pamoja na shughuli mbalimbali za maendeleo ya Parokia yetu, ni ushuhuda wa wazi wa imani yenu thabiti na upendo kwa Kanisa.

1. Maendeleo ya Kiroho na Kijamii
Tangu kuanzishwa kwa Parokia yetu, tumekuwa na ndoto na dhamira ya kujenga Parokia imara kiroho, kijamii, kiuchumi, na kimazingira. Leo hii ndoto hiyo imeanza kujidhihirisha machoni petu, tunamshukuru Mungu kwa hatua kubwa tulizofikia.

Kwa neema ya Mungu, Parokia yetu ina Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK) 75, ambazo zimekuwa msingi imara wa maisha ya kiroho, kijamii, na utume wa Kanisa.

Jumuiya hizi ni mahali pa kukuza imani, kuombeana, na kusaidiana kama familia ya Mungu.

Vilevile, tunashuhudia vyama vya kitume vikikua na kufanya kazi kubwa za kichungaji na kijamii. Ushiriki wenu katika vyama hivi ni alama ya uhai wa Parokia na moyo wa utume miongoni mwa waamini. Kwa haya yote, tunapaswa kusema, "Mungu ni mwema, tena ni mwaminifu!"

2. Maendeleo ya Miundombinu
Katika upande wa maendeleo ya miundombinu, napenda kuwapongeza sana kwa kazi kubwa na ya kujitolea mliyoifanya na mnayoendelea kuifanya. Ni wazi kwa macho yetu sote kuwa Parokia imepitia hatua nyingi:

- Tulianza na Kanisa la kwanza kwa msaada wa Shirika la Wamisionari wa Consolata, na baadaye, kwa nguvu zetu, tumeweza kujenga Kanisa kubwa na zuri la sasa linalotumika kwa Ibada na sala.
- Tumejenga nyumba ya kwanza ya Mapadre, na sasa tunajenga nyumba mpya ya Mapadre, hatua ambayo inaonesha kuimarika kwa Parokia yetu siyo tu kiroho bali pia kimazingira kwa ajili ya huduma endelevu kwa watu wa Mungu.

Jengo hili jipya la Mapadre ni alama ya matumaini, upendo, na imani ya pamoja kwamba tunataka kuwa na huduma bora na ya karibu kwa wanaparokia wetu na vizazi vijavyo.

3. Shukrani kwa Moyo wa Kujitoa
Ninapenda kutoa shukrani za pekee kwa kila mmoja wenu kwa moyo wa kujitolea, kutoa sadaka, zaka, na michango mingine kwa ajili ya maendeleo ya Parokia. Ushirikiano wenu unaendelea kuwa mfano mzuri kwa Parokia nyingine, na unathibitisha kuwa tukiungana kwa pamoja hakuna

linaloshindikana.
Kwa kweli, mnaonesha upendo wa dhati kwa Parokia, na nina hakika kuwa Mungu ataendelea kuwabariki na kuwaongezea kila mlichojinyima kwa ajili ya kazi yake.

4. Mwito wa Kuendeleza Umoja na Mshikamano
Ninawaomba tuendelee kushikamana, kuombeana, na kusaidiana kama familia moja ya Mungu. Tukiendelea kuunganisha nguvu, sala, na sadaka, naamini tutafanikisha malengo yetu yote kwa utukufu wa Mungu na kwa ajili ya kizazi kijacho.

Tuendelee kuwa watumishi waaminifu wa Kristo, tukitimiza wajibu wetu kwa bidii na furaha.

Hitimisho na Baraka
Kwa moyo wa dhati kabisa, ninaendelea kuwaombea baraka tele kutoka kwa Mungu:

- Awajalie afya njema na amani ya moyo.
- Awaongezee upendo na mshikamano.
- Awajalie mafanikio katika maisha yenu ya kila siku, pamoja na familia zenu.
- Awajaze Baraka tele za Mbinguni.

Tuzidi kuwa Parokia hai, yenye kushirikiana kwa upendo na mshikamano, tukitumikia na kushuhudia Injili ya Kristo kwa matendo yetu.

Mungu awabariki sana!

Baba Paroko

Parokia ya Bikira Maria Consolata – Makabe

Pongezi na Shukurani

Kwanza kabisa, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Parokia yetu ya Bikira Maria Consolata Makabe kufikia kimaendeleo hapa ilipo. Historia nzima ya Parokia ya Makabe inaonesha kuwa Mungu alikuwa na mpango mkubwa kuhusu Parokia hii na hivyo ni furaha kubwa kuona yote yaliyopo na yanayoendelea katika Parokia hii ya Makabe. Kwa hali hiyo tunawapongeza wale wote walioshiriki katika kufanikisha yote tunayoyaona katika Parokia ya Makabe, Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Tanzania. Tunatambua kuwa ushiriki wao mzuri na wa kujitolea ndio uliofanikisha yote maana Wanamakabe walitumia rasilimali zao kwa ajili ya maendeleo na kukua kwa Parokia yao ya Makabe.

Kwa namna ya kipekee, pongezi ziwafikie Maaskofu wetu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam na Mapadre wetu wa Parokia ya Makabe wa sasa na waliotangulia kwa kufanya kazi kubwa na iliyotukuka. Hakika mchango wao ndio kiini cha maendeleo yaliyopo leo katika Parokia ya Makabe. Wote hao, yaani, Maaskofu na Mapadre kwa namna moja au nyingine walikuwa sambamba na safari ya Mama Makabe kuelekea ambako leo tunamfurahia kwa maendeleo makubwa yaliyopatikana kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja. Kimsingi, kuwapo kwa usimamizi wao kumesababisha mafanikio yote maana hawakuwa kikwazo katika kuijenga Makabe yetu.

Kuna usemi wa Kiswahili unaosema, "Usione vyaelea, vimeundwa". Kwa namna ya pekee tunatambua sana jitihada na moyo wa imani na upendo wa wamisionari wa Shirika la Consolata na Shirika la MMI ambao waliianzisha na kuiendeleza Makabe kama historia inavyobainisha. Waconsolata (inasimuliwa kuwa) walianza kufika Makabe wakati mazingira yakiwa bado magumu na hakukuwa na miundombinu rafiki kama vile barabara ya maana na hivyo

kulazimika kutembea kwa miguu, lugha ngumu ya mawasiliano na kadhalika. Pamoja na yote hayo walilianzisha Kanisa la Bwana na leo hii linaendelea. Shirika la MMI wao waliipokea Makabe kutoka Parokia ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu Mbezi Mwisho Mazulu ikiwa haina fedha za kuendesha Parokia lakini walisimama kidete na kuendelea hadi tunapofurahia makubwa ya Parokia ya Makabe. Hii ni kazi ya mikono yao (Waconsolata na MMI), tuwapongeze, tuwashukuru na tuendelee kuwaenzi kwa kulitumikia Kanisa la Bwana, milele na milele, Amina.

Kwa umuhimu mkubwa tunapenda kuwashukuru wale wote waliokubali kuhojiwa na kutoa taarifa mbalimbali walizozifahamu na kuwa nazo. Tunajua wapo wengi sana ila kwa kuwabainisha wachache ni pamoja na Paroko Baba Pd. A. Amalraj, Paroko Msaidizi Baba Pd. Robin, aliyekuwa Paroko Msaidizi ambaye sasa amehama Baba Pd. A Kamtu na wajumbe wote wa Kamati Tendaji ya Parokia. Taarifa nyingi zilipatikana kutoka kwao.

Tunawashukuru Makarani na Waratibu wa Ofisi ya Parokia, yaani, Bi. Lucy Mwenda na Bi. Witnes Mallya walikuwa watu muhimu sana na walisaidia kupatikana kwa nyaraka kulingana na maelekezo waliyopewa na uongozi. Vilevile, tunapenda kuwashukuru Mzee Justine Msika maarufu kwa jina la Baba Ndele, Mzee Paul Luanda na Bwana Deo Chuwa kwa kutoa kumbukumbu mbalimbali za Makabe. Kwetu sisi waandishi tunawaona kuwa watu wenye uelewa na kumbukumbu kubwa kuhusu mambo ya Makabe. Wametoa taarifa ambazo ni muhimu na zilikuwa hazijaandikwa kokote au nyaraka zake hazieleweki ziliko. Wamekuwa na kumbukumbu nyingi sana za harakati mbalimbali za maendeleo ya Makabe. Kwa ujumla ni Fahari sana kuwa na watu hao na wengine wa aina yao.

Aidha, shukurani ziende kwa watu wengine waliosaidia kukamilisha kuandika kitabu hiki cha Fahari Yetu. Kati ya hao ni Dkt. Innocent Kangalawe aliyepitia na kutoa maoni ya msingi ya kitabu hiki. Vilevile, tunamshukuru Mheshimiwa Wakili Msomi Gasper Tluway na Mwl. Arbogast Kanuti waliopitia na kutoa maoni katika kukiboresha na kukiimarisha kitabu hiki.

Mwisho si kwa kuhitimisha ila ni kwa mtiririko na mfululizo tunapenda kutoa shukurani za pekee kwa Bwana Richard Mtambi, Mhariri Mkuu wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) aliyehariri lugha katika kitabu hiki. Amesaidia sana kuondoa matumizi mbalimbali yasiyo sahihi ya maneno ya Kiswahili. Pia, amesaidia kunyoosha sentensi na kuzifanya zisomeke kwa usahihi zaidi na hivyo kuleta utamu wa taarifa zinazohusika. Aidha, tunawashukuru sana wengine wote waliosaidia kukamilika kwa kitabu hiki kwa njia ya kupitia na kutoa maoni yao. Vilevile, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa ushirikiano mkubwa tulioupata kutoka kwa familia zetu. Pamoja na kututia moyo lakini pia wamekuwa wakishiriki katika hatua mbalimbali za uandishi zikiwamo kupendekeza mambo ya kuyaandika na aina ya taarifa zinazotakiwa, kupitia mswada na kurekebisha makosa ya kiuandishi na hivyo kufanikisha azma ya kuandika historia hii. Kwa kuhitimisha, tungeomba tuweke bayana kuwa upungufu wowote uliomo katika kitabu hiki hauwahusu hawa wote waliotajwa bali ni wa waandishi wa kitabu hiki.

Dosteus Lopa

Antipacy Shinyambala

SURA YA KWANZA

Utangulizi

Maelezo ya Usuli

Kitabu hiki kimeandikwa ili kuwapatia Wanamakabe na wasomaji wengine picha kamili ya Parokia ya Makabe kwa kuelezea historia ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe ikianzia mwanzo jinsi Makabe ilivyokuwa kabla na baada ya kuwa Parokia. Moja ya mambo muhimu ni kuelewa jina kamili la Parokia hii ambalo ni Bikira Maria Consolata Makabe ila limezoeleka kufupishwa na kutumika kama Parokia ya Makabe. Aidha Parokia ya Makabe kwa sasa ni jina kubwa na ni miongoni mwa majina yanayotajwa sana katika ngazi ya juu kutokana na ufanisi wake mkubwa na kwa kipindi kifupi.

Masuala mengi yameandikwa katika kitabu hiki ikiwamo namna Wanaparokia ya Makabe walivyoshiriki katika harakati za maisha ya kiroho na mikakati ya kuiendeleza Parokia ya Makabe tangu awali kabisa miaka ya kati ya 1970, baadaye miaka ya 1980 na kuendelea miaka ya 1990 hadi miaka ya 2000 kuja miaka ya 2010 hadi hii ya 2020. Kitabu kinaonesha aina na hatua mbalimbali za maendeleo na kuweka kumbukumbu ya historia nzuri ya Parokia ya Makabe. Historia ya Parokia hii ya Makabe imeanzia mbali hadi kuwa Parokia iliyotoa Parokia nyingine tatu ndani ya muda mfupi sana wa utume. Hii ni habari njema na ya kujivunia kwa maendeleo hayo ya muda mfupi hivi.

Kitabu kimekwenda mbali na kimeainisha harakati mithilika za maendeleo ambapo ndani yake kuna mchango wa viongozi na

mbinu mbalimbali zilizotumika kuendeleza Parokia ya Makabe. Ingawa kitabu hakijaweza kutaja mambo yote na kuwataja watu wote walioshiriki, kimefanikiwa kuyagusa na kuyabainisha mambo makubwa yaliyomo Parokini Makabe ambayo Mwenyezi Mungu amewajalia Wanaparokia ya Makabe kuyafanikisha ikiwamo mikakati mizuri ya kufikia malengo ya maendeleo. Kwa kifupi kitabu kimebainisha namna mipango na mikakati ilivyopangwa na kusimamiwa ili kuleta maendeleo yaliyokusudiwa. Aidha, kitabu kimeainisha ushirikiano na urafiki mzuri uliopo katika Parokia ya Makabe ukiwajumuisha Maaskofu, Mapadre, Viongozi wa Halmashauri ya Walei, Walei wenyewe na Vyama vya Kitume.

Mungu ni mwema maana mengi yametendeka na kuendelezwa hata Wanamakabe kuipenda na kuifurahia Parokia yao. Inafikia mahali au wakati Parokia ya Makabe imekuwa sehemu ya kujifunza kwa Parokia nyingine kwa mambo na maendeleo endelevu. Kitabu hiki kwa uzito mkubwa kabisa kimeandika kuhusu maendeleo yenye kuweka alama kubwa kwa taifa la Mungu yaliyofanyika Parokiani Makabe ndani ya miaka 14 tangu kuwa Parokia kamili ambayo ni ujenzi wa Kanisa la Parokia na Parokia zilizozaliwa toka Parokia ya Makabe. Kitabu kimemalizia kwa kuandika masuala ya matoleo kwa ajili ya kujitegemea na maadhimisho ya miaka 10 ya Parokia ya Makabe yaliyofanyika mwaka 2020.

Katika kufanikisha kuandika na kuhariri kitabu hiki kidogo cha *Fahari Yetu*, taarifa mbalimbali zilitafutwa na kutumika. Taarifa hizo zilipatikana kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo kupitia nyaraka mbalimbali za Parokia na kwenye mitandao, pamoja na kuwahoji watu mbalimbali maarufu na

mashuhuri wakiwamo Paroko (wa sasa na aliyemtangulia). Wengine waliohojiwa ni Viongozi wa Halmashauri ya Walei wa Parokia wa sasa (Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi na Mwekahazina), baadhi ya viongozi wa HWP waliokwisha maliza muda wao, Katekista Mstaafu, Makatekista wa sasa, Wajumbe wa Kamati za Parokia (Ujenzi na Sherehe), Watumishi wa Ofisi ya Parokia, na Wanaparokia mbalimbali. Baada ya kufanikiwa kuzipata taarifa, takwimu na picha mbalimbali za watu, vitu na matukio, kitabu kiliandikwa na kusanifiwa kama unavyokisoma sasa. Mpangilio wa kitabu umewekwa kulingana na mtiririko wa masuala muhimu ya Parokia ya Makabe.


Mahali ilipo Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Parokia ya Makabe ipo ndani ya eneo la utawala la Kata ya Mbezi Louis na Mtaa wa Makabe na makao makuu yake yako kwenye makutano ya Barabara ya Msumi na ya Msakuzi. Kimipaka kwa sasa (wakati kitabu hiki kinaandikwa) Parokia ya Makabe imepakana na Parokia kadhaa kama ifuatavyo:

- Kusini Mashariki: Makabe imepakana na Parokia ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu Mbezi Mwisho Mazulu
- Kusini: Makabe imepakana na Parokia ya Peter Clavery Mbezi Louis
- Kusini Magharibi: Makabe imepakana na Parokia ya Mshikamano
- Magharibi: Makabe imepakana na Parokia ya Pande
- Kaskazini: Makabe imepakana na Parokia ya Msumi
- Kaskazini Mashariki: Makabe imepakana na Parokia ya Tegeta ‘A’

- Mashariki: Makabe imepakana na Parokia ya Simon Stock Mbezi Mageti

Parokia ya Makabe inafikika kwa barabara za lami, vumbi na changarawe kutoka pande zote za Parokia zilizopakana nazo. Kutoka Barabara ya Morogoro kuna barabara mbili ambazo ni ile inayoanzia Barabara ya Goba na nyingine ni ile inayoanzia kwenye mzunguko wa makutano ya barabara pale Mbezi Mwisho ikipitia Madukani, GR, Child in the Sun na kufika Makabe njia panda. Kutoka Barabara ya Goba unaweza kufika Makabe kwa kupitia barabara ya kwa Robert, Aureke hadi Makabe. Pia, unaweza kupitia Kituo cha Tegeta 'A' kwa Bedui kupitia Kavimbirwa hadi Makabe. Barabara ya Madale unaingilia Madale, Darajani, Msumi, Kavimbirwa hadi Makabe. Barabara ya Mpigi Magoe kupitia Pande – Msakuzi, Mikoroshini hadi Makabe. Kutoka Mshikamano kupitia kwa Paulo, Mikoroshini hadi Makabe.



Ramani ya Mahali ilipo Parokia ya Makabe

Mandhari

Maeneo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe ni ya miinuko na miteremko na maeneo machache yakiwa tambarare. Uoto uliopo Makabe ni wa mchanganyiko wa miti ya asili na ya kupandwa. Hata hivyo, kutokana na watu kuendelea kuongezeka kwenye maeneo ya Makabe sambamba na shughuli za kibinamu, maeneo mengi yenye uoto wa asili yamekuwa yakijengwa nyumba za makazi na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Ujenzi unaoendelea kwa kasi kubwa kadiri miaka inavyokwenda unabadilisha kwa kiasi kikubwa mandhari kutoka kwenye mapori na kuwa makazi na majengo mengine. Hata hivyo, nyumba nyingi za Makabe zinazungukwa na uoto wa kijani kwa muda mrefu wa mwaka. Zipo zilizozungukwa na mipingo, migomba, miarobaini, milonge na miti mingine ya matunda kama miembe, michungwa, mipapai na mifenesi kwa kuitaja kwa uchache. Hii yote inaifanya Makabe ivutie sana kwa kipindi kirefu cha mwaka na hivyo kuwafanya wakazi wake kufurahia mandhari hiyo ya kuvutia.

Huduma za kijamii na kiuchumi

Maeneo haya ya Makabe kwa ujumla yana huduma chache sana za kijamii na kiuchumi. Kama ilivyoelezwa hapo juu Makabe inahudumiwa na barabara za lami, vumbi na changarawe ambazo wakati wa masika zile za vumbi na changarawe zimekuwa hazipitiki kwa urahisi. Hivyo, gharama za usafirishaji wa bidhaa na watu zimekuwa kubwa siku zote na hata kufanya gharama za kuishi Makabe kuwa juu kidogo. Kwa upande wa makazi Makabe ina aina mbalimbali za huduma hiyo yaani nyumba binafsi na za kupanga.

Huduma nyingine ni huduma za afya ambapo vipo vituo binafsi kadhaa vya kutolea huduma hizo. Kwa ufupi, kuna maabara, zahanati na maduka ya dawa baridi na muhimu. Upande wa elimu kuna shule za chekechea, msingi na sekondari za serikali na za watu binafsi ambazo zinawahudumia wakazi wa Makabe na maeneo ya karibu. Parokia ya Makabe na Kanisa zima pia inatoa huduma ya elimu kwa ngazi za awali (chekechea) na ya msingi, lengo ni kuja kuwa shule ya msingi iliyokamilika na kutegemewa katika ukanda huu. Mwendelezo wa majengo ya shule ya Msingi unaendelea. Pia kuwa na shule ya sekondari. Mwendelezo wa majengo hayo katika eneo letu lililopo maeneo ya *Child in the Sun* (imeelezwa zaidi katika sura ya tisa ya kitabu hiki) yapo katika hatua inayoonekana wazi.

Aidha, eneo la Makabe lina huduma za mawasiliano. Mitandao ya aina yote ya simu inapatikana Makabe na hii imewezesha shughuli mbalimbali za Parokia zifanikiwe. Kwa upande wa huduma za maji safi na salama, nalo linaendelea vizuri kwani wakazi wengi wa Makabe wameunganishwa na mfumo wa maji ya DAWASA ingawa kuna changamoto ya mtiririko wa kutoka. Lakini pia wakazi wengi wa Makabe wanatumia maji ya mvua na maji ya kuuziwa na wauza maji (maboza). Kwa maeneo ambayo bado huduma ya maji safi na salama haijafika wakazi wake wanatumia njia mbalimbali ili kupata maji kwa matumizi yao ya kila siku.

Huduma zote zilizotajwa hapo juu ni huduma zinazoendeshwa na sekta zote mbili za umma na binafsi. Huduma hizo zimefanikiwa kuajiri watumishi na watoa huduma mbalimbali na kuwapatia kipato kwa ajili ya maisha. Ni imani yetu kuwa

huduma zote zikiboreshwa zaidi kama vile barabara ya lami itafanikisha Makabe kukua kwa kasi kubwa na kuwa sehemu nzuri sana ya kuishi na shughuli za kiuchumi.

SURA YA PILI

Historia ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Safari ya kuwa Parokia

Sura hii ya pili inabainisha mchakato wa safari ya kuwa Parokia ulianzia wapi na lini. Inaendelea kuelezea pia baada ya kuwa Parokia na mambo kadha wa kadha yaliyotokea.

Kituo cha Sala Makabe

Historia ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe inaanza wakati ikiwa bado Kituo cha Sala miaka ya kati ya 1970 ikiwa chini ya Parokia ya Ubungo-Msewe. Kutoka hapa Makabe hadi Ubungo msewe ni mbali na kwa kukadiria ni karibu kilometa 20 kwa kufuata Barabara. Na masimulizi yanasema kulikuwa haieleweki nani alikuwa anaenda Parokiani kwa kuwa hakukuwa na hali yoyote ya kufahamiana ya wakatoliki miaka hiyo ya 1970. Mmoja wa waamini hao ni Bibi Mwingira ambaye amekuwa Makabe tangu miaka hiyo ya 1970 ambaye alisema *"Parokiani Ubungo-Msewe kulikuwa mbali sana na waamini wa Makabe walikuwa hawaendi kusali Parokiani"*. Hali hii ilipelekea kujiuliza namna gani Makabe ilikuja kuanza na hadi kufikia kuanzisha Kigango na baadaye Prokia. Tunasimuliwa[5] kuwa Parokia ya Makabe ilianza katika

[5]Mzee Justine Msika na Mzee Paul Luanda walisimulia historia ya Makabe kwa kuwa walianza kuishi maeneo hayo muda mwingi lakini pia

miaka hiyo ya 1970 kwa jitihada za Wakatoliki wachache waliotambuana kwa njia isiyo rasmi wakati wa mapumziko ya jioni baada ya kazi zao za siku nzima. Masimulizi yanasema kuwa waamini walianza kujitambua kupitia kuimba nyimbo mbalimbali za Kilatini za Kanisa Katoliki. Yaani, baada ya kujiona wanaimba pamoja nyimbo wanazozifahamu wakaanza kuulizana na hapo ndipo wakatambuana kuwa ni Wakristo Wakatoliki. Kwa hiyo, baada ya mazoea hayo ya kuimba nyimbo za Kanisa waliona ni vema wakianzisha pia utaratibu wa kusali pamoja ambapo walianza kwa kusali nyumbani kwa aliyekuwa tayari kuwakaribisha wenzake wasalie kwake. Hii ilikuwa changamoto kiasi fulani maana waamini wakatoliki walikuwa wanakaa mbalimbali na kupelekea wengine kuchagua wapi waende kusali na hivyo wazo la kupata sehemu moja ya kusalia ilianza kuwaingia kidogo kidogo.

Changamoto hiyo ya waamini wa mwanzo wa Makabe ya kusali kwa kuzunguka iliendeleka kukua na waamini hawakuupenda na hivyo haja ya kupata sehemu moja ya kusalia iliongezeka na kuwa bayana kwa kila mmoja wao. Masimulizi yanasema baada ya wao wenyewe kwa wenyewe kuongelea suala la kupata sehemu moja ambayo wataitumia kusalia wakafanikiwa kupata sehemu ya kusalia kutoka kwa mmojawao aliyejulikana kwa jina la *Bwana Sylivesta Edwin Mwale* ambaye alikuwa maarufu kwa jina la *"My Boy"*. Sehemu hiyo ilikuwa karakana ya useremala ya huyo bwana *My Boy* na hivyo waamini wa mwanzo wa Makabe waliacha kusali kwa kuzungukazunguka. Kwa mujibu wa masimulizi ya Babu na

---

wamefanya kazi Kanisani Makabe kwa nyadhifa za Ukatekista na uongozi wa Kigango na baadaye Parokia.

Bibi Mwingira karakana hiyo ilikuwa usawa wa ukuta wa eneo la kanisa kati ya Kibanda cha walinzi na ukuta wa Mama Mkubwa. Alama iliopo sasa ni kisiki cha mti wa mwembe uliokuwepo hapo na kutolewa wakati wa kuendeleza eneo la Parokia. Kibanda kilikuwa cha paa mbili na lililoezekwa kwa bati chakavu. Ukubwa wa banda ulikuwa meta za mraba kati ya 12 na 16.

Moja ya maswali ya kujiuliza ni namna gani taarifa zilifika Parokiani Ubungo Msewe. Swali lingine Uongozi ulifanikiwaje kujua kuna waamini huko Makabe wanapambana na Imani yao? Tunasimuliwa kuwa baada ya muda fulani waamini wachache waliokuwa mara moja moja wanaenda kusali Parokiani siku za Dominika walitoa taarifa Parokiani na mpango ukawekwa wa kutembelea Makabe na kuona kinachoendelea. Padre wa kwanza kufika Makabe wakati huo ni Hayati Pd. Luciano Scaccia wa Shirika la Bikira Maria Consolata (IMC). Baada ya Parokia ya Ubungo Msewe kuona umoja na moyo wa Wanamakabe kwa Mungu wao waliamua mara moja kuifanya Makabe kuwa kituo cha sala na baadaye kuipa Makabe hadhi ya Kigango kutoka kuwa kituo cha sala. Haijasimuliwa vizuri kuwa ilikuwa mwaka gani kwa mara ya kwanza Padre Luciano Scaccia – IMC alifika Makabe kwa mara ya kwanza.

Kupanda hadhi na kuwa Kigango cha Makabe

Baada ya kupata eneo la kusalia inasimuliwa kuwa watu wakapata mwamko zaidi na taarifa zikafanikiwa kufika Parokiani ambapo Mapadre, hasa Mh. Padre Luciano (IMC) akaamua kuitembelea Makabe na kuanzisha Kigango kwa jina la shirika lake la Bikira Maria Consolata (inakadiriwa ilikuwa

kati ya mwaka 1978 na 1980). Baada ya kuanzisha Kigango Parokia ya Ubungo-Msewe ilimweka Katekista wa kwanza Ndugu Xavery ili aweze kusimamia na kufanya shughuli za kitume katika Kigango cha Makabe kama ilivyobainishwa na Mzee Justine Msika maarufu kwa jila la Baba Ndele. Baada ya miaka kupita na mahitaji ya kichungaji kuongezeka Mzee Justine Msika aliteuliwa kuwa Katekista msaidizi na kuusaidia uongozi wa Halmashauri ya Walei Kigango cha Makabe.

Kutokana na kuanzishwa kwa Kigango cha Makabe huduma za kichungaji za Mapadre zilianza kupatikana. Waamini wa kigango cha Makabe walikuwa wanatoka eneo lote la kiutawala la Makabe, Msumi na Pande (kiserikali Pande imezoeleka kwa jina la Msakuzi). Eneo hili lilikuwa na idadi ndogo ya Wakatoliki na pia miundombinu na maendeleo mengine yalikuwa madogo sana. Tunasimuliwa na mzee Paul Luanda aliyeanza kuishi Makabe miaka ya kati ya 1990 kuwa maeneo hayo yalikuwa mashamba na mapori huku makazi ya watu yakiwa machache sana.

Kupanda Hadhi na kuwa Parokia ya Makabe

Kulingana na jiwe la uzinduzi wa Parokia, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, aliyekuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Julai 10, 2010 aliizindua rasmi Parokia mpya ya Makabe chini ya somo wake Bikira Maria Consolata. Askofu Mkuu wa Jimbo aliikabidhi Parokia mpya ya Makabe kwa Shirika la Wamisionari la Mary Immaculate (MMI). Shirika la MMI likamteua Mheshimiwa Padre Anthony Muthu kuwa Paroko wa kwanza na kufuatiwa na Mheshimiwa Padre Amaladoss na baada ya kuhama akaletwa Paroko wa tatu Mh. Pd. Amalraj kama inavyooneshwa kwenye Jedwali la

1. Parokia ya Makabe ilitangazwa rasmi kuwa Parokia tarehe 7 Julai, 2010 katika Misa ya Upadrisho iliyofanyika siku hiyo katika viwanja vya Msimbazi Centre.

Jedwali la 1: Maparoko, Maparoko Wasaidizi, Masista na Makatekista kati ya 2010 hadi 2022

Mwaka	**Paroko**	**Paroko Msaidizi**	**Makatekista**
2010 – 2014	Pd. Anthony Muthu	Pd. Ignas	Kat. Steven Msigwa
		Pd. Pushparaj	Kat. Lucresia Mwingira
		Pd. Amaladoss	Kat. Joseph Mgani
2014 – 2019	Pd. C. Amaladoss	Pd. Denis	Kat. Julius Mtanda
		Pd. Alex	Kat. Joseph Mapunda
		Pd. Ladislaus	Kat. Adolph Nkwera
		Pd. Absalom	
		Pd. Serva	
		Pd. Chinnadurai	
2020 -	Pd. Appavu	Pd. Reagan	Kat. Julius

2025	Amalraj		Mtanda
		Pd. Anthony Sami	Sr. Remigia - OSB
		Pd. Pari	Sr. Aneth – OSB
		Pd. Alberto Kamtu	Sr. Evarista – OSB
		Pd. Robbin	
		Pd. Anthony	

Jedwali la 2: Parokia zilizosimamia Kigango cha Makabe kabla ya kuwa Parokia kamili

Mwaka/miaka	**Chini ya Parokia**	**Shirika simamizi**
1978 - 2000	Mt. Paulo Mtume Ubungo-Msewe	Shirika la Wamisionari wa Consolata
2000 - 2007	Mt. Peter Xavery Mbezi Louis	Shirika la Wamisionari Wakarmeli
2007 - 2010	Mt. Theresia wa Mtoto Yesu Mbezi Mazulu	Shirika la Wmisionari Wakarmeli

Vigango vya Parokia ya Makabe

Wakati Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anaizindua Parokia ya Makabe aliipatia Parokia hii Vigango viwili ambavyo ni Kigango cha Mt. Benedicta wa Msalaba, Msumi na Kigango cha Mt. Yohane Maria Muzey, Tegeta 'A' ambacho kilihamishiwa kuwa Kigango cha Makabe kutoka

Parokia ya Bikira Maria Mama wa Huruma – Mbezi Beach. Baada ya miaka miwili yaani mwaka 2012 kilizaliwa Kigango kipya cha Pande katika eneo la Msakuzi ambako kulikuwa na kituo cha sala (eneo ambalo lilitolewa kwa hisani na Hayati Mhe. Benjamin William Mkapa – Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na hivyo kufanya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe kuwa na Vigango vitatu. Vigango hivyo vitatu kwa sasa (Machi 2025) wakati kitabu hiki kinakamilishwa kuandikwa vimepanda hadhi na kuwa Parokia kamili kama inavyobainishwa kwenye Jedwali la 3. Aidha, unaweza kusoma zaidi kuhusu kuzaliwa kwa Parokia hizo kutoka katika Vigango vya Parokia ya Makabe katika sura ya nne ya kitabu hiki.

Jedwali la 3: Parokia zilizokuwa Vigango vya Parokia ya Makabe yaani Msumi, Tegeta 'A' na Pande

Parokia	**Somo wa Parokia**	**Hadhi yake wakati kitabu kinaandikwa**	**Mwaka uliopandakuwa Parokia**
Msumi	Mt. Benedikta wa Msalaba	Parokia	2018
Tegeta 'A'	Mt. Yohane Marie Muzey	Parokia	2020
Pande	Bikira Maria Imaculata	Parokia	2021

Miaka 15 sasa (Machi 2024) tangu kuwa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe imeendelea kukua katika utume kwa miaka 14 na miezi 9 yaani takribani miaka 15 sasa tangu kupanda hadhi Julai 2010. Miaka hiyo ni michache kulinganisha na Parokia za zamani za Jimbo Kuu la Dar es Salaam lakini ni kielelezo kizuri na cha kujivunia kuwa Kanisa la Makabe linaendelea kukua kwa miaka yake ya utume na uchungaji. Hatua nyingi za maendeleo zimepigwa kwa kipindi hiki kama inavyoandikwa katika sura za kitabu hiki kidogo. Kwa hiyo, miaka hiyo ni mingi maana mambo mengi yamefanyika na Mungu siku zote aendelee kutukuzwa kuiwezesha Parokia yetu ya Bikira Maria Consolata Makabe kusonga mbele.

Kwa uhalisia unapoitazama miaka hii kumi na miwili ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe, lazima ugeuke nyuma halafu uanze kuvuta hisia eneo hili ambalo lilikuwa kichuguu na sasa lina mwonekana wa kisasa kabisa. Mambo mengi yamekwenda kwa kasi yake kuanzia huduma za kitume na kichungaji ambapo zimeimarika sana hapa Parokiani Makabe. Sakramenti zimetolewa na zinaendelea kutolewa kuanzia Ubatizo, Komunio, Kipaimara, Kitubio na Ndoa na miaka michache ijayo tunatarajia kuanza kuona Sakramenti za Daraja Takatifu la Upadre zikitolewa katika Parokia na hii ni kutokana na kuwa na waseminari wengi zaidi ya 30 walioko katika seminari mbalimbali, yaani, Seminari Ndogo na Seminari Kuu kwa ajili ya kusomea na kujiandaa kuwa Mapadre.

Maeneo ya Kanisa yamendelea kuboreshwa na kuwa sehemu nzuri zaidi ya kupatia huduma za kitume na kichungaji na hivyo kuwa mahali pa chemchemi za Neema na Baraka. Idadi kubwa ya Wanaparokia na Waamini Wakatoliki imeonekana kupata huduma hizo Makabe. Ni jambo la kumshukuru Mungu ambaye amewezesha Parokia hii ya Bikira Maria Consolata Makabe kukua na kuendelea kitume na kichungaji, tunazidi Kumsifu, Kumshukuru na Kumtukuza kwa hatua tuliyoifikia huku tukiomba Kutakatifuzwa naye.

Huduma za Kichungaji Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Katika kuangazia historia ya Parokia ya Makabe, ni muhimu kutathmini utoaji wa huduma za kiroho na kichungaji katika Parokia hii. Awali, wakati Makabe ikiwa bado ni Kigango, huduma za kichungaji zilipatikana kupitia Maparoko na Mapadre waliokuwa wakihudumu katika Parokia mbalimbali. Mwanzoni, huduma hizi zilitolewa kutoka Parokia ya Ubungo-Msewe, kisha kutoka Parokia ya Mbezi Louis, na hatimaye katika miaka ya mwisho kabla ya kuwa Parokia kamili, huduma zilipatikana kutoka Parokia ya Mbezi Mwisho – Mazulu.

Kwa msingi, Mapadre kutoka Parokia mama walihusika kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa huduma za kichungaji katika Kigango cha Makabe, pamoja na vigango vingine vya Parokia. Mwanzo, huduma hizi zilitolewa na Mapadre kutoka Parokia ya Ubungo-Msewe, kisha kutoka Parokia ya Mbezi Louis, na hatimaye kutoka Parokia ya Mbezi Mwisho – Mazulu.

Kutokana na hali hiyo, ibada za Misa Takatifu na huduma nyingine maalumu zilifanyika kwa uhakika zaidi siku za Dominika. Ibada za katikati ya juma au sikukuu maalum zilifanyika kwa nadra, kulingana na mazingira na upatikanaji wa Mapadre. Hali hii ilisaidia kuweka msingi thabiti wa maendeleo ya kiroho na kichungaji katika Makabe, hatua iliyosaidia kukua hadi kuwa Parokia na baadaye katika ukuaji wa Parokia yenyewe.

Baada ya kuwa Parokia huduma za kiroho na kichungaji zikaongezeka kwa kuwa Parokia ilikuwa na Mapadre wawili Parokiani (Paroko na Paroko Msaidizi) ambao waliweza kufanikisha ongezeko la huduma kwa Wanaparokia. Mapadre hao walikuwa na utaratibu wa kuadhimisha Misa Takatifu kila siku na siku za Dominika Misa Takatifu nne (4). Hii imesababisha Wanaparokia kuweza kusali Misa Takatifu kila wanapohitaji. Aidha, Mapadre wamekuwa na kawaida ya kuadhimisha Misa Takatifu kwenye ngazi ya JNNK na Kanda ambapo Sakramenti Takatifu nazo zimekuwa zikitolewa na kutoa baraka za nyumba. Kwa kifupi, baada ya kuwa Parokia kumekuwa na uhakika wa kuwepo kwa huduma za kiroho na kichungaji kila siku kadiri zinavyohitajika na taratibu za Kanisa. Utaratibu wa maadhimisho ya Misa Takatifu ni huu ufuatao:

1. Jumatatu hadi Ijumaa: Misa Takatifu moja inayoanza saa 12:30 asubuhi. Isipokuwa:

i. Siku ya Alhamisi: Siku ya Alhamisi ya Kwanza ya Mwezi huwa ni siku ya Kuabudu Ibada na Baraka Kuu inayoadhimishwa jioni saa 11 na kufuatiwa na Misa Takatifu.

ii. Siku ya Ijumaa: Wakati wa Kwaresma huwa kuna Ibada ya Njia ya Msalaba saa 11 jioni (pia wakati wa kipindi cha Kwaresma huwa kuna Ibada ya Njia ya Msalaba kila siku saa 12:00 asubuhi) na kufuatiwa na Misa Takatifu.

2. Siku ya Jumamosi: Siku hiyo imetengwa kwa ajili ya Misa Takatifu za kufungisha Sakramenti Takatifu ya Ndoa na pia Misa katika ngazi ya JNNK na Kanda.
   i. Pia siku za Jumamosi asubuhi ni siku maalumu za kusali ibada za kawaida za JNNK na Kanda.
   ii. Na tena kila Jumapili ya mwisho wa mwezi ni siku ya semina ya Parokia ambayo hufanyika wakati wa Maadhimisho ya Misa Takatifu.
3. Siku za Dominika: Misa Takatifu nne (4) kama ifuatavyo:
   i. Misa Takatifu ya kwanza huanza saa 12:00 asubuhi
   ii. Misa Takatifu ya pili huanza saa 01:30 asubuhi
   iii. Misa Takatifu ya tatu huanza saa 03:00 asubuhi ambayo inawalenga zaidi vijana na hivyo ni maarufu kwa jina la Misa Takatifu ya Vijana
   iv. Misa Takatifu ya nne huanza saa 04:30 asubuhi ambayo inawalenga zaidi watoto na hivyo ni maarufu kwa jina la Misa Takatifu ya Watoto
4. Dominika ya mwisho wa mwezi imewekwa Misa Takatifu ya jioni kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa na wazee. Misa hiyo huanza saa 10:00 jioni.

Aidha, kulingana na mahitaji na mwongozo wa Baba Paroko wakati mwingine kumekuwa na Misa Takatifu zaidi ya hizo kwa mfano Misa Takatifu za Ndoa, wafu au Misa Takatifu za maombi maalumu Parokiani au katika JNNK na Kanda.

Huduma nyingine muhimu sana ni kubariki nyumba wanazokaa waamini wa Parokia ya Makabe. Wanaparokia ya Makabe wanaona fahari sana kwa huduma ya kubarikiwa nyumba zao. Hii huduma ni muhimu sana na inagusa imani ya waamini katika jamii iliyojaa mitazamo na mapokeo tofautitofauti ya kiimani. Zoezi hilo huondoa hofu za imani za giza na hivyo kuongeza kujiamini kwa wale wanaoishi katika nyumba zilizobarikiwa. Mpango huo wa ibada ya kubariki nyumba unafanyika kwa namna mbili tofauti:

a. Namna ya kwanza ni wakati wa maadhimisho ya Misa Takatifu katika ngazi JNNK na Kanda. Padre anayeadhimisha Misa Takatifu pia hubariki nyumba moja au chache katika JNNK na Kanda inayohusika.
b. Namna ya pili ni kupitia utaratibu wa kubariki nyumba za Wanaparokia wakati wa kipindi cha Pasaka. Mapadre hupanga siku mbili hadi tatu kwa juma katika majuma yote ya kipindi cha Pasaka na kupita kwenye nyumba za Wanaparokia kwa ibada fupi ya baraka ya nyumba. Uratibu ni wa JNNK na Kanda moja hadi nyingine ili kuondoa changamoto ya kurudia rudia au kuruka eneo mojawapo. Mpango huo wa kubariki nyumba za Wanaparokia ulianza wakati wa Paroko wa kwanza Pd. Anthony Muthu na kuendelezwa na Maporoko waliofuata.

Huduma zingine za kiroho na kichungaji

Tukiacha Misa Takatifu kumekuwa na huduma nyingine nyingi za kiroho na kichungaji ndani ya Parokia ya Makabe ambazo zimekuwa zikitolewa na Mapadre wetu. Huduma hizo ni kwanza kabisa utoaji wa sakramenti mbalimbali kwa wahitaji hasa wagonjwa majumbani na pia hospitalini.

Waamini huomba huduma ya Padre kwa ajili ya watu wao. Utaratibu wa kawaida wa Kanisa ni kuomba kupitia JNNK kwa kujaza fomu ambayo itafikishwa Parokiani kupitia Makatekista na mara moja Mapadre huenda kutoa huduma inayohusika. Siku ya kutembelea wagonjwa hao na kupatiwa huduma za kiroho ni kila siku ya Jumanne ya kila juma.

Huduma nyingine ya kiroho na kichungaji inayotolewa ni misaada kwa wahitaji kupitia Shirika la Mtakatifu Vincent wa Paulo. Misaada hii hujumuisha chakula kinachotolewa kila mwisho wa mwezi, ambapo tangazo hutangazwa kanisani ili kuhakikisha wahitaji au wawakilishi wao wanafika kupokea msaada husika.


Mbali na chakula, misaada mingine hutolewa kulingana na mahitaji maalum, kama vile fedha, nguo, sabuni, na mafuta ya kupakaa, hasa katika kipindi cha Kwaresima na sikukuu kubwa za Kanisa. Katika kipindi cha Kwaresima, waamini huchanga michango ya fedha inayokusanywa Parokiani kama sehemu ya ushiriki wao katika Matendo ya Huruma kwa wahitaji. Mara nyingi misaada hii huelekezwa katika kituo cha Child in the Sun.

Aidha, waamini wa Parokia ya Makabe, wakifuata utaratibu unaosimamiwa na Parokia, pia hufanya matendo ya huruma katika hospitali za Tumbi na Bochi. Usimamizi wa misaada hii hufanywa na vyama vya kitume au JNNK, huku uongozi wa Parokia ukifahamishwa kwa ajili ya kutoa idhini na kufuatilia utekelezaji wake.
Wanaparokia wa Makabe pia wamewahi kutoa misaada kwa shule na vituo vya kulelea watoto wahitaji kama vile Mbagala

kwa Akina Dada Wadogo na Visiga, pamoja na magereza kama Segerea. Katika vituo hivi, misaada inayotolewa hujumuisha vyakula kama sukari, mchele, na maharagwe, ili kusaidia kuboresha maisha ya wahitaji.

Masista wa Kwanza Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Katika historia ya Parokia ya Makabe kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake, mwaka 2020 Parokia ilipata Masista wa Shirika la Masista la Wabenediktini OSB (wa Ilimiwaa) wa kutoa huduma za kitume Parokiani. Kumbukumbu za Parokia zinaonesha Aprili 2020 ndio shirika hilo la Wabenediktini OSB lilitoa Masista wawili ambao ni Sista Aneth Msigwa – OSB ambaye ni Katekista na wa pili ni Sista Remigia Mwigune OSB ambaye ni msimamizi wa Sakristia. Wakati akiwatambulisha Masista hao siku ya Dominika ya Matawi ya mwaka 2020 Paroko Pd. Amalraj Appavu alibainisha kwa kusema, *"Kwa mara ya kwanza Parokia yetu imepata Masista na hivyo kutimiza shauku ya muda mrefu ya Wanamakabe ya kuwa na Masista, ni jambo la furaha na kumshukuru Mungu sana"*. Wanaparokia walionesha furaha kubwa kwa kupata Masista wa kuhudumia Parokia ambao wamekamilisha mpango mkakati wa Parokia uliobainishwa katika kitabu cha Mwongozo wa Viongozi wa Kanisa (2016) wa kutafuta Shirika la Masista ili kufanya kazi ya utume Parokiani Makabe.





Picha: Masista wa kwanza kutumikia Parokia ya Makabe. Kutoka kushoto ni Sr. Aneth Msigwa, Sr. Remigia Mwigune na Sr. Evarista Mligo wa Shirika la Wabenediktini (OSB).

Muda mfupi baada ya kuwapata Masista hao, yaani, tarehe 27 Juni 2020, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi, alitangaza Pande kuwa Parokia Teule, kama ilivyoelezwa katika kitabu hiki. Kutangazwa kuwa Parokia Teule kulihusisha juhudi za

kujenga na kuimarisha miundombinu na mifumo mbalimbali ili kufikia hadhi kamili ya kuwa Parokia.

Miongoni mwa masuala ya msingi yaliyopewa kipaumbele ilikuwa kuimarisha idara ya mafundisho ya dini na liturujia, ambayo ni nguzo muhimu za uwepo wa Parokia. Kwa kutambua umuhimu huo, Sista Aneth Msigwa alihamishiwa Pande ili kusaidia katika ujenzi wa misingi hiyo na kuhakikisha kuwa Parokia Teule ya Pande inafikia vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kupanda hadhi. Ni muhimu kuelewa kwamba Paroko wa Parokia ya Makabe ndiye aliyekuwa msimamizi wa kitume wa Parokia Teule ya Pande katika safari yake ya kuelekea kuwa Parokia kamili. Muda wa kupanda hadhi kwa Parokia Teule ulitegemea kufikia viwango vinavyohitajika, jambo ambalo liliharakishwa kwa mchango wa Sista Aneth.

Ili kuziba pengo lililoachwa na Sista Aneth, mwezi Mei 2021, Parokia ya Makabe ilimpokea Sista mwingine, Sista Evarista, kutoka Shirika hilo hilo la Wabenediktini OBS. Sista Evarista alianza kazi kwa bidii na ari kubwa, akijikita zaidi katika mafundisho ya dini kwa watoto na vijana. Juhudi zake ziliimarisha zaidi mafundisho ya dini yaliyokuwapo, na matokeo yake yalionekana wazi katika ushiriki mkubwa wa watoto na vijana katika madarasa ya Jumapili. Aidha, alihamasisha watoto kushiriki kwa wingi katika ibada, wakiimba na kusoma masomo kwa ufasaha siku za Dominika, hivyo kuongeza uhai wa kiroho na ushiriki wa waamini katika liturujia.

Parokia ya Ubungo-Msewe chimbuko la Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe ipo katika eneo la Mbezi Louis, takribani kilometa nne (km 4) kutoka makutano ya Barabara ya Morogoro na Goba. Eneo hili lote, kuanzia Kibamba hadi Kimara, awali lilikuwa chini ya Parokia kongwe ya Ubungo-Msewe. Hivyo, Parokia ya Makabe, pamoja na parokia nyingine zote zilizoko kati ya Ubungo Msewe na Kibamba, zina asili moja kutoka Parokia hiyo ya zamani ya Ubungo Msewe.

Kabla ya Makabe kuwa Parokia kamili, eneo la Mbezi Louis lilikuwa tayari lina Kigango cha Mt. Peter Clavery, ambacho kilikuwa chini ya Parokia ya Ubungo-Msewe. Mwaka 2000, Kigango hiki kilipandishwa hadhi na kuwa Parokia ya Mt. Peter Clavery Mbezi Louis, na baadaye kikafanikiwa kutoa vigango vingi ambavyo leo hii vimepata hadhi ya kuwa Parokia kamili[6]. Parokia hizo ni:

1. Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe
2. Bikira Maria wa Mateso Msakuzi
3. Mt. Yohane Paulo II Mshikamano
4. Mt. Theresa Benedikta wa Msalaba Msumi
5. Mt. Theresia wa Mtoto Yesu Mbezi Mwisho-Mazulu
6. Mt. Yohane wa Msalaba Malamba Mawili
7. Mt. Augustino Temboni
8. Mt. Monika Matosa
9. Mt. Rita wa Kashia Temboni
10. Mt. Ambrosi Tagaste

[6] Kitabu cha Historia ya Parokia ya Mt. Peter Clavery Mbezi Louis cha mwaka 2012

11. Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili Mavurunza
12. Mt. Yohane Maria Muzeeyi Tegeta 'A'
13. Bikira Maria Imakulata Pande
14. Mt. Nicholaus wa Torentino Msingwa
15. Mwenyeheri Antonio Rosmini Mpiji Magohe
16. Bikira Maria Imakulata Goba Matosa
17. Mt. Simon Stock Mbezi Mageti

Mbali na parokia hizi, kuna pia vituo vya kichungaji kama Child in the Sun na Agape Center ambavyo vinatoa huduma mbalimbali za kiroho na kijamii kwa jamii inayozunguka. Ukuaji huu wa Parokia katika eneo la Mbezi Louis na vitongoji vyake ni kielelezo cha maendeleo ya Kanisa Katoliki na juhudi za wachungaji na waamini katika kuimarisha huduma za kichungaji na kiroho kwa waamini.

SURA YA TATU

Harakati Mithilika za Maendeleo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Uongozi na Harakati za Kufanikisha Maendeleo

Uongozi wakati Makabe bado Kituo cha Sala

Katika mazungumzo na wazee pamoja na Wanaparokia maarufu wa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe, imebainika kuwa moja ya nguzo muhimu zilizochangia maendeleo makubwa ya Parokia hii ni uongozi thabiti wa waamini wa eneo hilo. Tofauti na maeneo mengine ambako maendeleo ya kichungaji yalitegemea zaidi juhudi za wamisionari, Makabe iliweza kusonga mbele kwa kuwa na viongozi wenye maono, waliojitolea kwa dhati, na waliokuwa na shauku ya dhati ya kuendeleza maisha ya kiroho na kijamii.

Uongozi wa awali haukuanzishwa kwa utaratibu rasmi wa kanisa bali ulijitokeza kwa mfumo wa watu waliokuwa tayari kujitoa kuongoza na kuratibu shughuli mbalimbali huku wengine wakiunga mkono juhudi zao. Katika harakati hizi, Ndugu Bwana Sylivesta Edwin Mwale, maarufu kama *'My Boy,'* alijitokeza kuwa mmoja wa viongozi wa kwanza wa Makabe. Kwa moyo wa kujitolea, alitoa sehemu ya ardhi yake ili kuwezesha kuanzishwa kwa kituo cha sala, hatua ambayo ilikuwa msingi wa safari ya Makabe kutoka kuwa kituo cha sala hadi kuwa Kigango, na hatimaye kupanda hadhi na kuwa Parokia kamili ya Bikira Maria Consolata Makabe.

Mbali na kupata eneo, viongozi wa mwanzo walifanya juhudi kubwa za uraghabishi na ushawishi kwa viongozi wa Parokia mama ili kuhakikisha kuwa kituo cha sala cha Makabe kinatambuliwa rasmi na kupatiwa huduma muhimu za kiroho. Masimulizi ya Baba Ndele yanaeleza jinsi viongozi hao walivyojitahidi kuimarisha mawasiliano na uongozi wa Parokia, jambo lililosaidia kuanza rasmi kwa huduma za kichungaji katika eneo hilo. Hatua hizi zote zilikuwa msingi imara wa maendeleo yanayoendelea kushuhudiwa hadi sasa katika Parokia ya Makabe.

Uongozi wakati ikiwa Kigango cha Makabe

Kilipoanzishwa Kigango cha Makabe, uongozi wake uliimarika zaidi kwa kumpata Mwenyekiti wa kwanza ambaye pia alikuwa Katekista wa kwanza, Bwana Xavery. Aliungwa mkono na msaidizi wake, Mzee wetu Baba Ndele, aliyeshika nafasi ya Makamu Mwenyekiti na Katekista Msaidizi wa Kigango cha Makabe. Uongozi huu ulifanya kazi kubwa katika kuhakikisha ukuaji wa jumuiya ya Wakatoliki wa Makabe na ushiriki wao katika masuala mbalimbali ya Kanisa.

Moja ya mafanikio yao makubwa yalikuwa kuongeza idadi ya waamini na kuhakikisha kuwa Wakatoliki wa Makabe wanapata sakramenti mbalimbali kadiri ilivyowezekana. Walihamasisha na kuendesha mafundisho ya dini kwa watu waliotaka kubatizwa na kwa wale waliokuwa wakijiandaa kupokea Sakramenti Takatifu ya Komunio ya Kwanza, Kipaimara, na Ndoa.

Pia, uongozi huo ulikuwa kiungo muhimu kati ya Kigango cha Makabe na Parokia mama ya Ubungo-Msewe. Wao ndio waliokuwa wakipeleka taarifa kutoka Makabe na kupokea maelekezo kutoka Parokia ili kuhakikisha ushirikiano thabiti kati ya Kigango na Parokia. Katika kipindi hicho, changamoto ya mawasiliano ilikuwa kubwa, kwani hakukuwa na teknolojia ya kisasa ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hali hii iliwalazimu viongozi hao kusafiri kwa miguu au kutumia mabasi ya mjini kwa safari ndefu na ngumu kwenda Parokiani.

Kwa mujibu wa simulizi za Baba Ndele, ilikuwa katika kipindi cha uongozi huu ambapo wamisionari wa Shirika la Consolata, kwa kushirikiana na waamini wa Makabe, walihamasisha maendeleo zaidi ya Kigango, hatua iliyoimarisha msingi wa safari ya Makabe kuwa Parokia kamili.

Wanamakabe kuwa ndani ya Uongozi wa Juu wa Parokia

Wakati Makabe ilipokuwa bado ni Kigango, ilifanikiwa kuwa na Wanamakabe waliokuwa viongozi katika ngazi za Kamati za Utendaji za Parokia za Mtakatifu Peter Claver Mbezi Louis na Mtakatifu Theresia wa Mtoto Yesu Mbezi Mwisho Mazulu. Miongoni mwao ni Mzee Paul Luanda, aliyekuwa Katibu wa Parokia ya Mt. Peter Claver kati ya mwaka 2004 – 2006, na Bwana Deo Chuwa, aliyeshikilia nafasi ya Katibu wa Parokia ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu kati ya mwaka 2007 – 2010.

Viongozi haw awa zamani wanabainisha kuwa nafasi zao katika uongozi wa juu wa Parokia zilikuwa na mchango mkubwa kwa Kigango cha Makabe. Kupitia nafasi hizo, walipata fursa ya kujifunza masuala muhimu ya utawala wa

Parokia, jambo ambalo lilisaidia katika kupanga mikakati madhubuti ya kupandisha hadhi ya Kigango cha Makabe kuwa Parokia.

Moja ya mafanikio makubwa ya uongozi wao ni kuelewa vigezo na mahitaji muhimu ili Kigango kiweze kupata hadhi ya Parokia. Pia, walitambua umuhimu wa waamini kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Kigango kwa hali na mali. Ili kufanikisha hilo, uongozi uliweka mkazo katika kuelimisha na kuhamasisha waamini, kuwajenga katika utayari wa kuchangia maendeleo ya Kigango. Kwa ujumla, viongozi hawa, kwa nyakati zao, walifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha na kuwaandaa Wanamakabe, kuhakikisha kuwa mchakato wa kupandisha hadhi ya Kigango cha Makabe kuwa Parokia ulikuwa thabiti na wenye mafanikio.



Picha: Mzee Paul Luanda aliyekuwa Katibu wa Parokia ya Mt. Peter Clavery na baadaye Katibu Mkuu wa kwanza wa Halmashauri ya Walei Parokia ya Makabe.

Vilevile, uongozi wa Kigango cha Makabe, mbali na kufanikisha kuweka misingi imara ya maendeleo ya kiroho, uliweza pia kwa mara ya kwanza kumleta Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam kuadhimisha Misa ya Kiaskofu katika historia ya Makabe. Ilikuwa katika kiangazi cha mwaka 2008 ambapo Baba Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, aliyekuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, alifika Makabe kuadhimisha Misa Takatifu na kutoa Sakramenti ya Kipaimara kwa waamini 86.

Tukio hili lilikuwa la kihistoria na la kipekee, kwani kwa kawaida viongozi wa juu wa Kanisa huadhimisha Misa katika ngazi ya Parokia, na mara chache sana katika ngazi ya Kigango. Ujio wa Kardinali Pengo Makabe ulikuwa ishara ya kutambua juhudi kubwa za viongozi wa Kigango katika kujijenga na kuimarisha utendaji wake. Aidha, hatua hii ilikuwa moja ya mafanikio muhimu yaliyosaidia kuharakisha mchakato wa kupandisha hadhi ya Kigango cha Makabe na hatimaye kuwa Parokia kamili.

Mbali na hayo, uongozi wa Kigango uliendelea na mikakati ya maendeleo kwa kushirikiana na Marafiki wa Makabe, wakiwemo viongozi wa Kanisa kama Mh. Padre Albert Kamtu wa Shirika la Wamisionari wa Maria Imakulata (MMI). Padre Kamtu alitoa mchango mkubwa kwa kuwashauri, kuwaongoza, na hata kusaidia mawasiliano muhimu yaliyowezesha kufanikisha malengo ya Kigango.

Juhudi hizi za pamoja zilipelekea ujenzi wa miundombinu muhimu, ikiwa ni pamoja na upanuzi wa jengo la kanisa la mwanzo na ujenzi wa nyumba ya kwanza ya Mapadre. Wanamakabe walionyesha mshikamano wa hali ya juu kwa kujitolea kwa hali na mali, wakichangia fedha, vifaa vya ujenzi, na nguvu kazi ili kuhakikisha maendeleo yanapiga hatua (walithibisha Mzee Paul Luanda na Bwana Deo Chuwa).

Kwa kifupi, viongozi wa wakati huo waliweka msingi thabiti wa maendeleo, wakieneza dhana ya *"Maendeleo kuletwa na Wanamakabe wenyewe kwa kujitoa kwa hali na mali."* Mfumo huu wa mshikamano na kujitolea umeendelea kuwa sehemu ya utambulisho wa Wanamakabe hadi leo.

Uongozi baada ya kuwa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Baada ya Makabe kupanda hadhi na kuwa Parokia utaratibu wa Kanisa wa kuwa na viongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia (HWP) ukachukua mkondo wake. Kwa hiyo kuanzia 2010 hadi hivi sasa na kuendelea kuna viongozi kama inavyoonekana katika Jedwali la 4.

Jedwali la 4: Viongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia (HWP) tangu kuanzishwa kwa Parokia

Na	Jina la Kiongozi	Nafasi
	2010 -2012	
1.	Sabas Massawe	Mwenyekiti HWP
2.	Lightness Sungula	Makamu Mwenyekiti HWP
3.	Paulo Luanda	Katibu HWP
4.	Anthony Njiku	Katibu Msaidizi
5.	Deo Chuwa	Mwekahazina HWP
	2012 – 2015	
1.	Antipacy Shinyambala	Mwenyekiti HWP
2.	Dennis Msafiri	Makamu Mwenyekiti HWP
3.	Adam Nyoni	Katibu HWP
4.	Pakomius Philipo	Katibu Msaidizi HWP
5.	Deo Chuwa	Mwekahazina HWP
	2015 – 2020	
1.	Antipacy Shinyambala	Mwenyekiti HWP
2.	Dennis Msafiri	Makamu Mwenyekiti HWP

3.	Gaspar Ngalu	Katibu HWP
4.	Adam Nyoni/ Joseph Massae	Katibu Msaidizi HWP
5.	Deo Chuwa	Mwekahazina HWP
	2020 – 2023	
1.	Antipacy Shinyambala	Mwenyekiti HWP
2.	Dennis Msafiri/Justine Ngowi	Makamu Mwenyekiti HWP
3.	Gaspar Ngalu	Katibu HWP
4.	Mariatheresa Gutta/Catherine Mwashilindi	Katibu Msaidizi HWP
5.	Remi Urio	Mwekahazina HWP
6.	Getrude Shayo	Mwekahazina Msaidizi HWP
	2023 – 2026	
1.	Justine Ngowi	Mwenyekiti HWP
2.	Osward Mramba	Makamu Mwenyekiti HWP

3.	Gaspar Ngalu	Katibu HWP
4.	Cecilia Swai	Katibu Msaidizi HWP
5.	Getrude Shayo	Mwekahazina HWP
6.	Antipacy Mallya	Mwekahazina Msaidizi HWP



Picha: Kamati Tendaji ya Parokia ya Makabe and iliyokuwa Kigango cha Pande Msakuzi katika picha ya Pamoja na Mha. Askofu Mkuu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi mara baada ya Maadhimisho ya Misa Takatifu ya Kutabaruku Kanisa na Altare 27 Juni. 2020: Mstari wa mbele kutoka kushoto ni Ndugu Antipacy Shinyambala, Mwenyekiti; Ndugu Dennis Msafiri, Makamu Mwenyekiti; Ndugu Gasper Ngalu, Katibu Mkuu; Bi.

Mariatheresa Gutta, Katibu Msaidizi; na Ndugu Remi Urio, Mweka Hazina.

Uongozi wa Parokia ya Makabe, baada ya kupandishwa hadhi kutoka Kigango, uliendeleza na kuboresha misingi iliyowekwa awali, hivyo kuchochea maendeleo makubwa. Mafanikio haya yalitokana kwa kiasi kikubwa na ushirikiano thabiti kati ya viongozi wa Parokia na wanaparokia, kwa lengo la pamoja la kuleta maendeleo endelevu. Ili kuhakikisha maendeleo haya yanaimarika kwa nyakati zote, uongozi wa Parokia umejikita katika mikakati ifuatayo:

1. Kuimarisha utawala bora, uwajibikaji, na uwazi katika maamuzi.
2. Kuwashirikisha waamini wa Makabe katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
3. Kuimarisha idara muhimu za Parokia, zikiwemo Liturujia, Mipango na Fedha, Elimu na Hamasa, pamoja na Ofisi ya Taarifa na Utunzaji wa Kumbukumbu, ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wanaparokia.
4. Kuandaa na kutekeleza sera zinazochochea maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na kimazingira.
5. Kuendesha semina na mafungo ya kiroho kwa waumini ili kuwajenga kiimani na kimaadili.
6. Kukuza na kuimarisha vikundi vya kiroho kama vile Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK), Legio Maria, WAWATA, VIWAWA, UWAKA, na Karimatiki Katoliki.
7. Kualika Mapadre, Masista, na wahubiri wageni kwa ajili ya mafundisho ya kina ya Imani na wajibu katika kamtumikia Mungu.

8. Kuendesha mikutano kati ya waumini na viongozi wa Kanisa ili kujadili masuala ya imani, maadili, na maendeleo ya Parokia.
9. Kuunda kamati maalum za kusimamia na kuratibu michakato ya miradi ya ujenzi yaani kamati ya Maendeleo, Kamati ya Mavuno na kamati ya Ujenzi.
10. Kuanzisha harambee na michango ya wanaparokia kwa ajili ya kufanikisha miradi ya maendeleo.
11. Kuwekeza katika teknolojia na mifumo ya kidijitali ili kurahisisha mawasiliano na utoaji wa huduma za Parokia.

Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa ni ujenzi wa Kanisa kubwa la Parokia, ambao ulianza mwaka 2011 na kukamilika mwaka 2020, kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni moja. Maendeleo mengine ni ujenzi wa Kanisa la Kuabudia lenye mapango (Grotto) ya Mama Bikira Maria na Mtakatifu Yosefu, pamoja na ujenzi wa ofisi mpya ya Parokia, maliwato, na nyumba mpya ya Mapadre.

Aidha, Parokia ilifanikiwa kupanua eneo lake kwa kupata ardhi zaidi kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo eneo linaloanzia lango kuu la uzio wa Kanisa hadi shule ya Parokia, pamoja na sehemu iliyo ndani ya kituo cha *Child in the Sun.*

Maendeleo mengine muhimu ni ununuzi wa gari la Parokia na kuanzishwa kwa shule inayotoa elimu ya awali na msingi, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kutoa malezi bora kwa watoto wa jamii ya Makabe. Mafanikio haya yote ni matokeo ya mshikamano na juhudi endelevu za uongozi wa Parokia pamoja na waumini wake.

Ushiriki wa Viongozi Wakuu wa Kanisa katika maendeleo ya Parokia

Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam

Mfumo wa uongozi wa Kanisa Katoliki unamfanya Mkuu wa Jimbo kuwa kiongozi wa juu wa Kanisa mahalia. Katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam, nafasi hii inashikiliwa na Mheshimiwa Askofu Mkuu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi, ambaye alianza kutumikia Jimbo mwaka 2018 kama Askofu Mkuu Mwandamizi. Mwaka 2019, Baba Mtakatifu Francis alimteua rasmi kuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Kabla yake, Jimbo Kuu la Dar es Salaam liliongozwa na viongozi mbalimbali, akiwemo Hayati Mwadhama Laurian Kardinali Rugambwa, ambaye aliongoza wakati Makabe ilipopandishwa hadhi na kuwa Kigango cha Parokia ya Ubungo Msewe. Baadaye, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo alichukua uongozi na hatimaye kumkabidhi Askofu Mkuu wa sasa, Mheshimiwa Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi. Historia inaonesha kuwa Mwadhama Kardinali Pengo, aliyelitumikia Jimbo Kuu la Dar es Salaam kuanzia mwaka 1999 hadi 2019, ndiye aliyeipandisha Makabe kuwa Parokia tarehe 10 Julai 2010.

Kwa masimulizi na taarifa mbalimbali zinaonesha kuwa mwaka 2008, Mwadhama Kardinali Pengo alitoa mwongozo na kuidhinisha upanuzi wa kanisa la kwanza, pamoja na ujenzi wa nyumba ya Mapadre. Mwaka 2010, aliidhinisha ujenzi wa kanisa kubwa, ambalo maelezo yake yamefafanuliwa kwa kina katika sura ya nne ya kitabu hiki. Kwa mujibu wa ushuhuda wa Bw. Deo Chuwa, aliyekuwa mmoja wa viongozi wa

Kigango cha Makabe, Mwadhama Kardinali Pengo alifanya vikao kadhaa na uongozi wa Kigango ili kuweka mkakati wa maendeleo na kuhakikisha Makabe inakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa Parokia.

Jimbo Kuu la Dar es Salaam limepata uongozi wa maaskofu mbalimbali waliotumikia kwa vipindi tofauti. Awali, maaskofu walioliongoza walikuwa wamisionari kutoka mataifa ya nje kabla ya Watanzania kuanza kulitumikia. Katika historia ya Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Askofu wa kwanza alikuwa Cassian Spiess wa Shirika la Wabenediktini (OSB), akifuatiwa na Askofu Thomas Spreiter wa shirika hilo hilo. Baadaye, uongozi uliendelea na Askofu Gabriel Zelger wa Shirika la Wakapuchini (Cap.), kisha Askofu Mkuu Edger Maranta wa Shirika la Wakapuchini (Cap.), ambaye ndiye aliyemkabidhi uongozi wa Jimbo Mkuu wa kwanza Mtanzania, Mwadhama Laurian Kardinali Rugambwa.


Wakati wa uongozi wa Askofu Mkuu Maranta, nafasi ya uaskofu msaidizi ilianzishwa kwa mara ya kwanza katika Kanisa Katoliki Tanzania, ambapo Padre Elias Mchonde wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam aliteuliwa kuwa Askofu Msaidizi wa kwanza wa Jimbo hilo mnamo tarehe 21 Septemba 1956. Baadaye, mwaka 1964, Askofu Mchonde aliteuliwa kuwa Askofu wa Jimbo jipya la Mahenge, akiwa ndiye askofu wa pili mzalendo kwa Kanisa Katoliki Tanzania.

Kwa muhtasari, Uongozi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam umekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Kanisa, ikiwemo kupandishwa hadhi kwa Kigango cha Makabe hadi

kuwa Parokia, sambamba na miradi mingine ya maendeleo inayolenga kuboresha maisha ya waumini.


Wafuatao kutoka kushoto ni Maaskofu waliotangulia kuliongoza Jimbo Kuu la Dar es Salaam:


1. Askofu Cassian Spiess (wa Shirika la Wabenediktini OSB)
2. Askofu Thomas Spreiter (wa Shirika la Wabenediktini OSB)
3. Askofu Gabriel Zelger (1920 - 1930, wa Shirika la Wakapuchini Cap.)
4. Askofu Mkuu Edger Maranta (1933 - 1969, wa Shirika la Wakapuchini Cap.)






Wafuatao ni Maaskofu Wakuu wazalendo wa Jimbo Kuu la Dar er Salaam akianzia na Mwadhama Laurian Kardinali Rugambwa, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo na Askofu Mkuu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi









Wafuatato ni Maaskofu ambao wamekuwa Maaskofu wasaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam kwa miaka tofauti tofauti akianza Askofu Elias Mchonde (1956-1964), Askofu Methodius Kilaini (2000 - 2009), Askofu Esebius Nzigilwa (2010 - 2020), Askofu Salitaris Libena (2010 - 2012), Askofu Titus Mdoe (2013 - 2017), Askofu Henry Mchamungu (2021 hadi sasa wakati kitabu hiki kinaandikwa) na Askofu Steven Msomba (2021 hadi Machi 2025 wakati kitabu hiki kinakamilishwa kiuandikwa).



Picha: Maaskofu Wasaidizi waliotumikia Jimbo Kuu ya Dar es Salaam kuanzia mwanzo hadi sasa wakati kitabu hiki kinaandikwa.

Mchango wa Maaskofu Wasaidizi kwa Parokia ya Makabe

Katika nyakati mbalimbali, Maaskofu hao walitembelea Parokia ya Makabe na kutoa huduma mbalimbali za kichungaji kwa wanaparokia ya Makabe. Shughuli muhimu walizoshiriki ni pamoja na:

1. Kuadhimisha Misa Takatifu na kutoa Sakramenti ya Kipaimara.
2. Kusaidia na kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa Kanisa jipya.
3. Kutoa miongozo na hamasa kwa wanaparokia kuhusu maendeleo ya Parokia.
4. Kusikiliza maoni, maswali na mawazo ya wanaparokia ambapo mengine walitolea ufafanuzi na mengine waliyachukua Kwenda nazo Jimboni.

Kumbukumbu Muhimu Kuhusu Maaskofu Wasaidizi

Moja ya kumbukumbu muhimu kuhusu mchango wa Maaskofu Wasaidizi kwa Parokia ya Makabe ni ahadi ya Mheshimiwa Askofu Eusebius Nzigilwa kuhusu suala la kupata Masista wa kufanya utume katika Parokia hiyo. Alipokuwa akijibu swali la Wanaparokia ya Makabe kuhusu uwezekano wa kupata Masista, aliwahakikishia kuwa uongozi wa Jimbo ulikuwa unashughulikia suala hilo kwa umakini ili kuhakikisha kwamba Parokia inapata msaada wa kitume kutoka kwa Masista.

Vilevile, Parokia ya Makabe inamkumbuka sana Mha. Askofu Eusebius Nzigilwa katika kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa Kanisa jipya. Moja ya kumbukumbu ni pale alipojibu risala ya Parokia kuhusu lini Kanisa litatabarukiwa, alieleza:
"Jimbo linaelewa juhudi zilizotumika, lakini linaendelea kuwatia moyo Wanaparokia ya Makabe kuongeza nguvu zaidi ili kukamilisha ujenzi, kwa kuwa si vizuri kutabaruku Kanisa huku ujenzi haujakamilika kabisa. Kukamilika kwa ujenzi kunajumuisha pia uwepo wa samani zote muhimu za Kanisa. Jimbo halitachelewa kulitabaruku Kanisa hili na linaendelea kuwafuatilia na kuwasimamia." Kauli hii iliendelea kuwahamasisha waamini wa Parokia kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa Kanisa linakamilika kwa viwango vinavyostahili.

Aidha, mnamo tarehe 3 Oktoba 2021, Mheshimiwa Askofu Henry Mchamungu aliadhimisha Misa Takatifu ya Kiaskofu na kutoa Sakramenti ya Kipaimara, kama inavyoelezwa katika sura ya nne ya kitabu hiki. Katika mahubiri yake, kama ilivyo desturi ya viongozi wa Jimbo, alihimiza Wanaparokia ya Makabe kujitoa kwa bidii katika kulitumikia Kanisa la Mungu bila kuchoka, akisisitiza umuhimu wa imani, mshikamano, na utume wa waumini katika maendeleo ya Parokia.

Uongozi wa Parokia na Mchango wa Maparoko

Tangu kuanzishwa kwa Parokia ya Makabe, Maparoko wote watatu waliowahi kuhudumu wamekuwa mstari wa mbele katika kusimamia maendeleo mbalimbali tunayoyaona leo. Maparoko hao ni:

1. Mheshimiwa Padre A. Muthu
2. Mheshimiwa Padre C. Amaladoss

3. Mheshimiwa Padre A. Amalraj (Paroko wa sasa wakati kitabu hiki kinaandikwa)

Katika vipindi vyao, **Maparoko hawa watatu** wameweka alama kubwa ya maendeleo katika Parokia ya Makabe, na juhudi zao zimeleta maendeleo ya kiroho na kijamii kwa waamini.

Mchango wa Mheshimiwa Padre A. Muthu

Mheshimiwa Padre A. Muthu, ambaye alikuwa Paroko wa kwanza wa Parokia ya Makabe, alianzisha miradi kadhaa muhimu ambayo imeendelea kuleta manufaa makubwa kwa Parokia hadi sasa. Miongoni mwa mchango wake mkubwa ni kuanzisha ujenzi wa Kanisa kubwa, ambapo alisimamia mradi huo hadi hatua ya kupauliwa. Juhudi zake zilihamasisha wanaparokia kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Parokia, na msingi aliouweka umewezesha kukamilika kwa ujenzi huo miaka iliyofuata.

Katika kupanua eneo la Parokia, Padre Muthu alisimamia upatikanaji wa ardhi zaidi kwa ajili ya maendeleo, ikiwemo eneo kutoka geti kuu la uzio wa Kanisa hadi mwisho wa jengo la Shule ya Bikira Maria Consolata, eneo la Kavimbirwa, na eneo la *Child in the Sun.* Upanuzi huu ulitoa fursa za kupanua huduma za kiroho na kijamii kwa wanaparokia, pamoja na kuimarisha miundombinu ya Parokia kwa matumizi mbalimbali.

Aidha, alianzisha mpango wa utoaji wa huduma za elimu ndani ya Parokia kwa kuanzisha Mfuko wa Elimu wa Parokia, ambao uliundwa kusaidia maendeleo ya elimu miongoni mwa watoto wa jamii ya Makabe. Mpango huu umeendelea kuwa

msaada mkubwa kwa familia nyingi zinazohitaji usaidizi wa kielimu kwa watoto wao.

Katika nyanja ya usafiri na usimamizi wa rasilimali, Padre Muthu alisimamia ununuzi wa magari mawili muhimu kwa Parokia. Gari aina ya *TATA Double Cabin Pick-Up* lilinunuliwa kwa msaada wa wafadhili baada ya kuandika andiko la mradi, na gari aina ya *Suzuki Escudo* lilinunuliwa kupitia michango ya waamini wa Parokia ya Makabe. Magari haya yalichangia sana katika kuboresha huduma za Parokia, hasa katika usafirishaji wa viongozi wa Kanisa na utekelezaji wa miradi ya kijamii na kiroho.

Mchango wa Padre Muthu uliweka msingi thabiti wa maendeleo ya Parokia, na miradi aliyoanzisha imeendelea kuimarika hata baada ya kipindi chake cha utumishi. Uongozi wake wa kujitolea na maono yake ya maendeleo vimeacha alama isiyofutika katika historia ya Parokia ya Makabe.



Picha: Padre Antony Muthu ndiye Paroko wa kwanza kufanya utume Parokia ya Makabe kuanzia 2010 hadi 2014.



Picha: Padre Ignas wa MMI aliyekuwa Padre wa Kwanza kusimama kama msimamizi na kiongozi wa Makabe kabla haijapanda hadhi na kuwa Parokia (2008-2010).

Mheshimiwa Padre C. Amaladoss

Mheshimiwa Padre C. Amaladoss ambaye alikuwa Paroko wa Pili tangu anzisha Parokia ya Makabe alisimamia maendeleo makubwa ya Parokia, hasa katika sekta ya ujenzi na kuimarisha mshikamano wa wanaparokia ya Makabe. Uongozi wake ulijikita katika kuhamasisha ushirikiano na kujitolea kwa wanaparokia ili kufanikisha maendeleo ya Parokia. Miongoni mwa mafanikio yake makubwa ni kuendeleza ujenzi wa Kanisa kubwa kwa kuwahamasisha wanaparokia kuchangia kwa hali na mali, ikiwemo fedha, vifaa vya ujenzi, na nguvukazi. Jitihada zake ziliwezesha kukamilika kwa sehemu kubwa ya Kanisa na kuweka mazingira bora ya ibada kwa wanaparokia.

Katika kusimamia rasilimali za Parokia, Padre Amaladoss aliongoza juhudi za kulipa deni la mkopo wa TZS milioni 340 kutoka Benki ya Mkombozi, mkopo uliotumika kununua eneo muhimu la ardhi parokiani kuanzia geti kuu la eneo la Kanisa hadi jengo la Shule ya Chekechea na Msingi ya Maria Consolata – Makabe. Hatua hii ilihakikisha Parokia inapanua huduma zake na kuwa na maeneo zaidi kwa maendeleo ya baadaye.

Aidha, alijikita katika kuimarisha mshikamano wa wanaparokia kwa kushirikiana vyema na viongozi wa Parokia, wafanyakazi, na waamini wote. Ushirikiano huu uliongeza kasi ya maendeleo ya Parokia, ambapo alifanikisha matumizi ya Kanisa kubwa, akionyesha ujasiri wa uongozi wake na uwezo wa kufanya maamuzi shirikishi. Mahusiano yake mazuri na Halmashauri ya Walei Parokia (HWP) yaliwezesha upatikanaji wa vifaa vya ujenzi kama vigae, marumaru, na vifaa vingine kwa bei nafuu kwa kushirikiana na Kamati ya Ujenzi.

Katika kuboresha mfumo wa uchangiaji Parokiani, alihamasisha mfumo bora wa utoaji wa zaka na mavuno kwa Parokia na Jimbo, jambo lililoleta ufanisi mkubwa katika michango ya waamini. Mbali na hayo, alibuni mawazo mapya ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Hospitali ya Parokia, wazo ambalo liliridhiwa na kuundwa Kamati Maalum ya utekelezaji chini ya Hayati Prof. Honest Ngowi. Pia, alipendekeza miradi ya kiuchumi kama shule ya Parokia na ujenzi wa maduka kwenye uzio wa Parokia ili kuongeza vyanzo vya mapato vya kudumu.

Katika sekta ya kiroho, Padre Amaladoss alihimiza mafundisho na semina kwa waamini kwa kuwaleta Mapadre mbalimbali kuadhimisha Misa na kutoa mafundisho siku za Jumapili. Pia, alimruhusu Padre Chinna, Paroko Msaidizi, kutumia karama zake, hasa kwa kuwa karibu na watoto, jambo lililochangia ongezeko la ushiriki wao katika Misa.

Kwa ujumla, uongozi wa Padre C. Amaladoss umeacha alama kubwa katika historia ya Parokia ya Makabe, kwani juhudi zake ziliimarisha miundombinu, mshikamano wa wanaparokia, na maendeleo ya kiroho na kijamii.



Picha: Padre C. Amaladoss ni Paroko wa pili kufanya utume Parokia ya Makabe kuanzia 2014 hadi 2019.

Mheshimiwa Padre A. Amalraj (Paroko wa sasa)
Baada ya Padre Amaladoss, Mheshimiwa Padre A. Amalraj alichukua usukani na kusimamia hatua za kuendeleza michakato ya maendeleo ya Parokia, akihakikisha kuwa miradi muhimu inakamilika na kuboresha huduma za kiroho Parokiani. Miongoni mwa juhudi zake zilikuwa ni kuimarisha na kuboresha zaidi mafundisho na semina za kiroho kwa kuwaleta Mapadre mbalimbali kuadhimisha Misa na kutoa mafundisho kila Jumapili. Aidha, alianzisha darasa la Biblia lililolenga kuwafundisha wanaparokia wa Makabe Neno la Mungu, hatua iliyosaidia kuongeza uelewa wa wanaparokia katika imani yao.

Katika nyanja ya miundombinu, Padre Amalraj alisimamia kukamilika kwa ujenzi wa Kanisa kubwa, ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa samani zake, na kusimamia ujenzi wa Kanisa la kuabudia pamoja na Groto la Mtakatifu Yosefu na Bikira Maria. Vilevile, alihusika katika ununuzi wa magari ya Parokia na shule ya Bikira maria Sonsolata, hatua iliyosaidia kuboresha ufanisi katika shughuli za Parokia na elimu.

Fanikio lingine kubwa chini ya uongozi wake Padre Amalraj ilikuwa ni ujenzi wa nyumba mpya ya Mapadre, hatua iliyoboresha mazingira ya makazi na utendaji kazi wa viongozi wa kiroho. Kwa upande wa elimu amesimama kidete na kuendeleza mradi wa elimu kwa kuanzisha ujenzi wa majengo ya shule katika eneo lililoko ndani ya kituo cha *Child in the*

Sun, jambo lililolenga kutoa fursa bora za elimu kwa watoto wa jamii ya Makabe.

Jambo jingine kubwa alilolifanya ni pale alipoboresha sherehe za somo wa Parokia kwa kuzifanya ziende sambamba na siku ya kumbukumbu ya kutabaruku Kanisa jipya la Parokia. Hii hatua imeleta mshikamano zaidi kati ya wanaparokia na kuongeza thamani ya kiimani katika Parokia ya Makabe.



Picha: Padre A. Amalraj ni Paroko wa tatu aliyeanza utume Parokia ya Makabe mwaka 2020 hadi wakati kitabu hiki Kinaandikwa.

Marafiki Mapadre na Wengine wa Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Tangu awali, uongozi wa Parokia ya Makabe umebarikiwa na marafiki wa dhati ambao wamechangia maendeleo yake kwa hali na mali. Hili limekuwa si tu bahati, bali pia mkakati madhubuti wa kuhakikisha ushirikiano wa karibu na wadau wa Parokia unaendelea kuzaa matunda.

Mh. Padre Luciano Scaccia (IMC): Mmoja wa marafiki wa kwanza kabisa wa Parokia ya Makabe ni hayati Mh. Padre Luciano Scaccia wa Shirika la Wamisionari wa Bikira Maria Consolata (IMC). Ingawa Padre Luciano alikuwa akihudumu katika Parokia ya Ubungo Msewe, ambapo Makabe ilikuwa sehemu yake wakati huo, ndiye aliyekuwa wa kwanza kuifikia Makabe, kutambua mahitaji yake, na kuchochea juhudi za maendeleo yake ya kiroho na kijamii.

Kwa moyo wa upendo na ari ya kimisionari, Padre Luciano alipenda Makabe kwa dhati na kuanzisha michakato iliyowezesha kuwa Kigango. Upendo wake kwa Makabe ulikuwa chachu muhimu, kwani bila yeye huenda Kigango kingeanzishwa mahali pengine au wakati mwingine tofauti na ule. Wanaparokia wa Makabe wanamkumbuka na kumheshimu Padre Luciano kama rafiki wa kwanza wa Parokia, ambaye alichochea mwendo wa maendeleo tunayoendelea kuyaona leo.

Urafiki huu wa kihistoria haukuishia kwa Padre Luciano pekee, bali umeendelezwa kati ya Parokia ya Makabe na Shirika la Consolata. Mpaka sasa, Mapadre kutoka Kituo cha Consolata Bunju huendelea kuja Makabe kutoa huduma za

kiroho, kudhihirisha mshikamano wa kimisionari ulioanzishwa miaka mingi iliyopita.

Kwa hakika, marafiki wa Parokia ya Makabe wamekuwa nguzo muhimu ya maendeleo yake. Ushirikiano huu umeimarisha imani, umoja, na ustawi wa wanaparokia, na kuendeleza urithi wa mapadre waliotangulia kwa vizazi vijavyo.



Picha: Pd. Luciano Scaccia IMC wa shirika la Bikira Maria Consolata na ndiye aliyeanzisha safari ya utume Makabe ikiwa

bado kituo cha sala na kuwa Kigango akitokea Parokia ya Ubungo Msewe.

Mh. Padre Albert Kamtu: Baada ya Makabe kuwa Kigango na miaka mingi kupita, mwaka 2008 Parokia ilipata rafiki mwingine muhimu—Mh. Padre Albert Kamtu wa Shirika la Wamisionari wa Maria Imakulata (MMI). Padre Kamtu, ambaye wakati huo alikuwa Paroko Msaidizi wa Parokia ya Kibangu, alileta mchango mkubwa katika maendeleo ya Makabe, hasa katika harakati za kupandisha hadhi kutoka Kigango kuwa Parokia kamili.

Historia ya Padre Kamtu na Makabe inaanzia mwaka 2004 alipojiunga na masomo ya Daraja Takatifu katika Seminari Kuu ya Peramiho. Wakati wa likizo ya Desemba 2005, alipumzika katika Kituo cha *Child in the Sun*, kilichopo Makabe na kusimamiwa na Shirika lake la MMI. Ndipo alipoanza kufahamiana na waamini wa Makabe, hususan Sabas Massawe na Qs. Patrick Tarimo, na hatimaye akajenga uhusiano mzuri na uongozi wa Kigango.

Baada ya kupewa Daraja Takatifu la Upadre, Padre Kamtu alirudi Tanzania kama mmisionari wa kwanza wa Shirika la MMI kuhudumu katika Parokia ya Kibangu. Kazi yake ya kichungaji ilimpa uzoefu mkubwa wa michakato na sera za Jimbo Kuu la Dar es Salaam kuhusu maendeleo ya Parokia na Vigango. Maarifa haya yalikuwa msaada mkubwa kwa wanamakabe, hasa katika juhudi za kupanda hadhi kuwa Parokia kamili.

Mchakato wa kupandisha hadhi Kigango cha Makabe ulikuwa mgumu, hasa kwa sababu Parokia mama ya Mtakatifu Theresia wa Mtoto Yesu - Mbezi Mwisho Mazulu, yenyewe ilikuwa changa na bado ilikuwa katika hatua za kujijenga. Changamoto hii ilifanya iwe vigumu kwa Makabe kupata msukumo wa kutosha wa kusimamia hoja ya kupanda hadhi. Katika mazingira haya, uwepo wa Padre Kamtu kama rafiki na mshauri ulikuwa wa thamani kubwa.

Katika juhudi hizo, Padre Kamtu alitoa msaada muhimu wa mawazo, ushauri, na mwongozo wa hatua za kuchukua ili kufanikisha lengo la Makabe kuwa Parokia. Alisaidia pia mawasiliano na viongozi wa Jimbo, ikiwemo kufanikisha mikutano kati ya uongozi wa Makabe na Katibu wa Jimbo, hatua iliyosaidia kurahisisha mchakato wa kupanda hadhi.

Kwa kifupi, urafiki wa Parokia ya Makabe na Padre Kamtu ulionyesha thamani kubwa ya ushirikiano na msaada wa watu wenye uzoefu. Leo hii, Padre Kamtu anabaki kuwa sehemu muhimu ya historia ya Makabe, na sasa akiwa Paroko Msaidizi wa Parokia ya Makabe, anaendelea kushiriki kikamilifu katika gurudumu la maendeleo ya Parokia ambayo alihusika kuianzisha.



Picha: Mh. Padre Albert Kamtu ambaye pia alikuwa Paroko Msaidizi wakati kitabu hiki kinaandikwa.


Historia ya Mheshimiwa Padre Albert Kamtu iliendelea kung'ara hata baada ya kuondoka Kibangu, hasa wakati alipokuwa Mkuu wa Shirika la Wamisionari wa Maria Imakulata (MMI) ulimwenguni kuanzia Novemba 2010 hadi Machi 2022. Katika kipindi hiki, Padre Kamtu alidumisha uhusiano wake wa karibu na Parokia ya Makabe, akiendelea kuwa rafiki wa dhati na msaidizi wa maendeleo ya Parokia.

Moja ya mafanikio makubwa aliyoyafanikisha wakati wa uongozi wake ni kumleta Askofu Mkuu Francis Kalist, aliyekuwa msimamizi na mshauri wa Shirika la MMI nchini India, kutembelea Tanzania na kufika Parokia ya Makabe mwaka 2015. Ziara hii ilikuwa na umuhimu wa pekee kwa Parokia ya Makabe, kwani ilikuwa mara ya kwanza kwa Askofu wa kiwango hicho kuitembelea Parokia hiyo.

Ingawa rasmi ilikuwa ni ziara ya kichungaji kwa ajili ya Shirika la MMI, kwa Parokia ya Makabe ilikuwa zaidi ya ziara ya kawaida. Askofu Mkuu Francis Kalist aliadhimisha Misa Takatifu na pia alishiriki katika mijadala ya maendeleo ya Parokia. Kwa moyo wa ukarimu, alichangia si tu mawazo, bali pia msaada wa kifedha ili kusaidia jitihada za maendeleo ya Parokia.

Tukio hili lilizidi kuimarisha nafasi ya Padre Kamtu kama mmoja wa marafiki wakubwa wa Parokia ya Makabe, akiwa mtu aliyekuwa tayari kuendeleza uhusiano wa kimisionari na kusaidia juhudi za kiroho na kimazingira katika Parokia. Hadi leo, mchango wake unahesabiwa kuwa wa thamani kubwa katika historia na maendeleo ya Parokia ya Makabe.

Mh. Padre Almachus Rwejuna: Rafiki wa tatu au aliyefuata ni Mh. Padre Almachus Rwejuna wa Jimbo Katoliki la Bukoba, ambaye alikuwa rafiki wa Parokia ya Makabe kuanzia mwaka 2017 hadi 2020, kipindi ambacho alikuwa anasoma shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ameacha alama kubwa katika kuamsha na kuimarisha imani ya waamini wa Makabe.



Picha: Pd. Almachus Rwejuna.

Baba Paroko wa pili wa Parokia ya Makabe, Mh. Padre Amaladoss, ndiye aliyemkaribisha na kushirikiana naye kwa ukaribu. Baadaye, Paroko wa tatu, Mh. Padre Almalarj, aliendeleza ushirikiano huo na Mh. Padre Almachius, ambaye alihudumu karibu kila Jumapili, akihubiri ama Parokiani Makabe au Kigangoni Pande (ambayo sasa ni Parokia ya Pande). Mchango wake mkubwa Padre Almachius ulionekana katika kuelimisha na kuhamasisha waamini wa Makabe kuhusu kulitambua, kulitumikia, na kulipenda Kanisa lao.

Katika mahubiri na semina alizoandaa kwa waamini na viongozi wa Walei, aliwahimiza Wanamakabe kuwajibika kwa Kanisa lao. Alikuwa akisema mara kwa mara: *"Huwezi kupenda*

kitu bila kukijali, kukisimamia, kukiboresha, na kukitumikia." Mafundisho yake yalivutia wengi, na kutokana na hilo, idadi ya waamini waliokuja kushiriki Misa za Jumapili iliongezeka. Hata waamini kutoka Parokia za jirani walihamasika kuja kusali Makabe kutokana na mafundisho yake yenye mguso wa kipekee.

Miongoni mwa mambo makubwa yanayokumbukwa na wanaparokia ya Makabe kuhusu utumisha wa Mh. Padre Almachus ni mamizi ya misemo yenye hekima na mafundisho makini katika mahubiri na semina zake. Baadhi ya misemo yake mashuhuri ni:

- *Usiogope kutoka, ogopa kuingia.*
- *Ukarimu unalipa.*
- *Hakikisha unakuwa sehemu ya historia ya Kanisa la Makabe.*
- *Miye nasema tu, ila Wanamakabe hampo hivyo.*
- *Hofu na shaka zikiongezeka, Imani inapungua.*
- *Mti hauli matunda yake.*
- *Mto haunywi maji yake.*
- *Hatulingani, ila Mungu ni Mwema.*
- *Bila chochote, huwezi kupata chochote.*
- *Kanisa siyo majani ya mti yakanyauka na kupukutika, ila angalia usije ukanyauka na kupukutika.*
- *Mungu hadhihakiwi.*
- *Mipango ya Mungu siyo ya kwetu.*
- *Padre ni wakili wa Yesu.*
- *Upekee katika ukawaida – unaweza ukaona msalaba ni kitu cha kawaida, lakini ndani yake umo upekee wa ajabu.*
- *Mkristo, chunga mawazo yako: mawazo hutengeneza fikra, fikra hutengeneza mipango, mipango hutengeneza matendo,*

matendo hutengeneza mazoea, na mazoea hutengeneza tabia na desturi ambazo zinaweza kuwa mbaya.

Kupitia mafundisho yake Mh. Padre Almachus aliwafanya Wanamakabe kuelewa na kutambua umuhimu wao katika Kanisa, huku akiwahimiza kujitoa kwa ajili ya kazi ya Mungu. Katika historia ya maendeleo ya Parokia ya Makabe, mchango wake unakumbukwa daima, kwani alichochea juhudi za waamini kuchangia maendeleo ya Parokia yao.

Mh. Padre Almachius atakumbukwa sana kwa wazo na pendekezo zuri na muhimu la kuanzisha ni **darasa la Biblia**, ambalo sasa limeanzishwa rasmi na Parokia ya Makabe. Mwalimu Albogast Kanuti ndiye kiongozi mkuu wa darasa hilo, akiongoza juhudi za kufundisha elimu ya Biblia kwa waamini wa Makabe.

Mchango wa Padre Almachus katika kuhamasisha na kuimarisha imani ya waamini utaendelea kukumbukwa daima. Wanaparokia ya Makabe wanaendelea kumshukuru na kumwombea baraka tele kutoka kwa Mungu Mwenyezi. **Amina.**

Marehemu Monsinyori Deogratius Hukumu Mbiku: Huyu ni mmoja wa Mapadre pendwa sana wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam kwa kuwa na uwezo mkubwa sana katika utume wake. Sisi Wanamakabe tulipata bahati ya kuwa naye karibu sana na alitupenda sana. Mara nyingi Mapadre wetu ambao kwa asili ni wa kimataifa kutoka India walihitaji mtu wa kuwasaidia masuala mbalimbali ikiwamo kufanya vizuri kiutume na

walimtumia sana Marehemu Monsinyori Mbiku kupata ushauri na mwongozo wa nini kifanyike.



Picha: Monsinyori Deogratius Hukumu Mbiku.

Baba huyu alifika mara kadhaa Parokiani Makabe kutoa huduma mbalimbali. Alifika mwaka 2016 (wakati huo Paroko alikuwa Pd. Amaladoss) kwa ajili ya kutoa semina ya Zaka na siku hiyo Misa ilikuwa moja tu. Yeye ndiye aliyeadhimisha Ibada ya Misa Takatifu na katika mahubiri yake alitumia saa moja kuwafundisha Waamini nini maana, asili na faida za kutoa zaka. Katika mafundisho yake alieleza kwa ufasaha sana kuwa nani alitakiwa kutoa Zaka, namna ya kutoa Zaka, nini hasara ya kutotoa Zaka/Zaka kamili. Alifundisha kwa mifano mingi kutoka kwenye maandiko Matakatifu na rejea zingine za kikanisa. Alikuja na vitabu vyake vya Zaka ambapo yote aliyokuwa anayafundisha yalikuwa yameandikwa mle. Aliyasema kama yalivyoandikwa, neno kwa neno, kituo kwa kituo na mstari kwa mstari, kipaji kikubwa na cha aina yake!

Pia, Paroko wetu wa sasa alimtumia sana kufanikisha Maadhimisho yetu ya miaka 10 ya Parokia. Baba Paroko alisikika wakati wa Maadhimisho ya Misa Takatifu ya Kutabaruku Kanisa letu jipya kuwa wakati anaendelea na maandalizi ya siku hiyo amekuwa na vikao mbalimbali na Baba Mbiku ili kupata mwongozo na ushauri wake. Pia, kuwa tayari kuja kuwa mratibu na kiongozi. Baba Paroko alikuwa anapata ushauri wa karibu sana kuhusiana na taratibu za wakati wa maandalizi ya uzinduzi n.k., wa Maadhimisho yetu ya miaka 10 ya Parokia na Kutabaruku Kanisa letu.

Mapadre wengine: Pia, kulikuwa na Mapadre wengine waliokuwa marafiki na wenye mapenzi makubwa kwa Parokia ya Makabe ambao walisaidia sana katika kazi za kitume na kichungaji akiwamo Pd. Benno Kikudo – aliyekuwa Dekano wa Dekania ya Kibaha, Pd. Vitalis Kassembo – Mkurugenzi wa Utume wa Walei, Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Pd. Komba wa Shirika la White Fathers, Pd. Jerome Mentoraj kutoka kituo cha *Child in the Sun*, Pd. Sabuni kutoka Parokia ya Manzese, Pd. Mgani wa Shirika la Waagustino, Pd. Kulwa kutoka Seminari Kuu ya Segerea, Marehemu Pd. Ngowi (Sauti ya Radi) wa Shirika la Damu Azizi, Pd. Msafiri (aliyekuwa kituo cha Agape) na Mapadre wengine wengi kutoka Seminari ya Visiga, Shirika la Kimisionari la MMI na Mapadre mbalimbali wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Makatekista: Nguzo Muhimu Ya Parokia Ya Makabe

Makatekista ni mhimili wa maisha ya kiroho na kichungaji katika Parokia ya Makabe. Mbali na kuwa walimu wa dini,

wao ni wachungaji wasaidizi wanaoshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Mapadre.

Tangu Makabe ikiwa bado ni Kigango, Makatekista wamechangia sana maendeleo ya Parokia, hususan katika kufundisha na kusimamia elimu ya dini na liturujia. Waamini wanaopokea Sakramenti Takatifu—kama Ubatizo, Kipaimara, Ekaristi, Kitubio, Ndoa, na Mpako wa Wagonjwa—hupata malezi na maandalizi yao kutoka kwa Makatekista, hivyo kusaidia kuhakikisha waamini wanajua na kuelewa imani yao. Uwepo wao hutoa msaada mkubwa kwa Mapadre, kuhakikisha ibada zinafanyika kwa mpangilio mzuri na waamini wanapokea huduma za kiroho ipasavyo. Kwa kifupi, Makatekista ni kiungo muhimu kinachowezesha Parokia ya Makabe kuendelea kukua kiimani na katika utume wake wa kueneza Injili.

Makatekista wanahusika moja kwa moja katika maandalizi na uendeshaji wa liturujia na Maadhimisho ya Misa Takatifu, iwe ni za Dominika, siku za juma, ngazi ya Kanda na JNNK, au Misa maalum za matukio mbalimbali. Wanaratibu mavazi ya kiliturujia, vifaa vya ibada, na usomaji wa masomo ya Misa, huku wakishirikiana na watumishi wa Altare na kusaidia waumini kushiriki kikamilifu katika ibada.

Katika historia ya Parokia, umuhimu wa Makatekista umedhihirika zaidi wakati wa sherehe na maadhimisho maalum kama Pasaka, Noeli, Pentekoste, na utoaji wa Sakramenti. Juhudi zao zilionekana wazi wakati wa Kutabaruku Kanisa na Altare ya Parokia ya Makabe mnamo 27 Juni 2020, pamoja na sherehe za Miaka 10 ya Parokia

tarehe 27 Desemba 2020, zilizofanyika chini ya uongozi wa Mhashamu Baba Askofu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Orodha ya Makatekista wa Parokia ya Makabe

1. Sylvester Edwin Mwale (maarufu kama My Boy) – Katekista wa kwanza, aliyefariki miaka ya 1980.
2. Xavery – Alihudumu hadi 1997 alipofariki dunia; pia alikuwa Mwenyekiti wa HW wa Kigango cha Makabe.
3. Justine Msika (Baba Ndele) – Alirithi nafasi ya Xavery, akiwa pia Makamu Mwenyekiti wa Kigango cha Makabe.
4. Aniseta Kinyaia – Alifuata baada ya Baba Ndele.
5. Marehemu Steven Msigwa – Katekista wa kwanza wakati Makabe ilipopewa hadhi ya Parokia.
6. Lucresia Mwingira – Mke wa Marehemu Katekista Msigwa, aliyeshika nafasi hiyo baadaye.
7. Joseph Mgani – Aliteuliwa baada ya Lucresia Mwingira.
8. Julius Mtanda (maarufu kama Katekista Babu) – Alihudumu pamoja na Joseph Mgani.
9. Aldofu Nkwela – Alipewa majukumu mwaka 2019 kama Katekista wa muda baada ya Joseph Mgani kuondolewa.
10. Sista Aneth Msigwa (OSB) – Aliteuliwa kuwa Katekista rasmi kuanzia Aprili 2020, akishirikiana na Julius Mtanda.
11. Sista Evarista – Aliteuliwa mwaka 2021 kusaidiana na Julius Mtanda baada ya Sista Aneth kuhamishiwa Parokia ya Pande.

Kwa miaka yote, Makatekista hawa wamefanya kazi kubwa ya kueneza Imani, kuwafundisha waamini, na kusaidia utoaji wa Sakramenti kwa watoto, wakatekumeni, na wanandoa. Ukatekista ni utume wa kujitolea unaoendeshwa kwa upendo mkubwa. Tunamshukuru Mungu kwa zawadi hii ya thamani ya Makatekista wetu. Mungu aendelee kuwalinda, kuwaongoza, na kuwabariki daima! Amina.

Mikakati na Michakato ya kufanikisha maendeleo

Ushiriki wa Vyama vya Kitume vya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Kwa mujibu wa Kitabu cha Mwongozo wa Viongozi wa Kanisa cha Parokia ya Bikira Maria Consolata – Makabe (2016), vyama vya kitume vinafafanuliwa kama *"mhimiili wa makuzi ya kiroho na nyenzo muhimu katika kurahisisha utoaji wa huduma, kukuza na kuimarisha imani za waamini."* Kutambua umuhimu huu, Parokia ya Makabe imevipa vyama vya kitume nafasi kubwa katika shughuli za maendeleo ya kiroho na kijamii. Vyama vya kitume vilivyopo Parokiani ni: WAWATA, UWAKA, VIWAWA, UKWAKATA, Karizmatiki Katoliki, Legio Maria, Mt. Anna, Mt. Vincent wa Paulo, Moyo Mtakatifu wa Yesu, Utoto Mtakatifu, CPT, Chama cha Wazee na Wastaafu cha Mtakatifu Agustino, Watumishi wa Altare, Mama Anna, na Rozari Hai.



Picha: WAWATA Parokia wakiwa katika picha ya pamoja siku ya safari ya Hija ambayo waliiandaa na kuiratibu.

Vyama vya kitume katika Parokia ya Makabe vimekuwa mstari wa mbele katika kuchangia maendeleo ya Parokia kwa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu kama vile kanisa, nyumba ya mapadre, na ofisi ya Parokia. Aidha, vimesaidia katika kuratibu shughuli za kiroho kama sala, hija, semina za kiroho, na utoaji wa mafundisho ya dini. Pia, vyama hivi vina mchango mkubwa katika kuhamasisha waamini kushiriki michango na kujitolea nguvukazi kwa kazi za maendeleo ya Parokia.

Ili kuendeleza na kuimarisha utume wa vyama hivi, Parokia inahimiza waamini kujiunga na kushiriki kikamilifu katika vyama vya kitume kwa mujibu wa kanuni na malengo yake. Kwa kufanya hivyo, wanaparokia wanachangia si tu katika

kuimarisha imani yao binafsi, bali pia katika huduma za kichungaji na maendeleo ya jumuiya kwa ujumla.

Ushirikishwaji wa Wanaparokia wa Parokia ya Makabe

Maendeleo makubwa yanayoonekana Parokiani Makabe yametokana na uongozi thabiti wenye mtazamo wa maendeleo, kama ilivyoelezwa katika Sura ya Tatu ya Kitabu cha Mwongozo wa Viongozi wa Kanisa cha Parokia ya Bikira Maria Consolata – Makabe (2016). Maparoko waliotumikia Parokia, yaani, Mh. Pd. Muthu, Mh. Pd. Amaladoss, na Mh. Pd. Amalraj, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Walei wa Parokia (HWP), wamefanya kazi kubwa kuhakikisha Parokia inapata maendeleo endelevu.

Jambo moja kubwa linaloendeleza maendeleo ya Parokia ya Makabe ni utaratibu wa kuwashirikisha Wanaparokia kwa njia na mbinu mbalimbali. Kwenye ushirikishwaji wa Wanaparokia Viongozi wa KTP walisema, *"Mbinu shirikishi imekuwa kinga na kigawe cha Wanamakabe kufikia mafanikio hayo. Ushirikishwaji unaanzia kutoka kuzalisha mawazo, kuchakata mawazo hadi utekelezaji wake. Kwenye vikao na mikutano ya ngazi mbalimbali waamini wanashirikishwa na wanapata nafasi ya kutoa maoni yao kupitia viongozi wao wa JNNK na Kanda".* Njia au mbinu hizo shirikishi ni pamoja na:

1. **Uongozi wa Karibu na Wanaparokia – Maparoko Mh. Pd. Amaladoss na Mh. Pd. Amalraj walitumia nafasi yao ya kichungaji kwa kuwatembelea Wanaparokia katika kaya zao. Katika matembezi hayo, walitumia fursa hiyo kuzungumza nao, kutoa ushauri wa kiroho, na kuwabariki. Pia, walipokea maoni na mawazo mbalimbali kutoka kwa waamini kuhusu**

maendeleo ya Parokia ya Makabe, hatua iliyochangia sana katika kuboresha mipango ya kichungaji na kijamii.

2. **Kukutana na Wanaparokia katika ngazi mbalimbali** – Uongozi wa Parokia ya Makabe umeweka utaratibu mzuri wa kuwafikia Wanaparokia katika maeneo wanayoishi ili kusikiliza mawazo na maoni yao kuhusu maendeleo yanayohitajika. Kifupi viiongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia wamekuwa wakikutana na Wanaparokia katika ngazi ya kaya, JNNK, na Kanda, jambo ambalo limeimarisha mshikamano wa kijamii na kiimani.
3. **Vikao vya kusikiliza na kukusanya mawazo** – Uongozi huandaa mikutano ya Wanaparokia kwa ajili ya kupokea maoni, kupanga malengo, na kuweka mikakati ya maendeleo.
4. **Kuunda kamati za usimamizi na utekelezaji** – Kamati mbalimbali zimeanzishwa kwa ajili ya kusimamia shughuli za Parokia kwa ushirikiano wa Wanaparokia. Viongozi wa Parokia wanakuwa na jukumu la kuratibu, huku majukumu ya utekelezaji yakifanywa na kamati hizi (Jedwali 5).

Jadwali la 5: Baadhi ya Kamati za kuratibu na kusimamia maendeleo Parokiani Makabe

Na	Jina la Kamati	Mradi au shughuli ya Maendeleo
1	Kamati ya Hamasa	Iliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 2010 ili kutoa elimu na kuwahamasisha Wanaparokia kujitoa kwa Mungu katika shughuli za maendeleo kuanzia ujenzi wa Kanisa kubwa la Parokia.

		Kamati hii ndiyo iliyotuibulia Mwenyeketi wa HWP wa sasa kwani alikuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa na kwa kupitia hamasa hizo watu wakamfahamu na ilipofika wakati wa uchaguzi mwaka 2012 alichaguliwa kuanzia kwenye Jumuiya yake, Kanda, Kigango (wakati huo) na hatimaye Parokia.
2	Kamati ya Ujenzi	Iliundwa rasmi kwa mara ya kwanza mwaka 2011 ikihusisha mchanganyiko wa wataalamu wa mambo ya ujenzi yaani wahandisi, mafundi ujenzi, wasambazaji vifaa vya ujenzi (wauzaji) na wachumi ili kusimamia ujenzi wowote Parokiani wakianzia na ujenzi wa Kanisa kubwa, choo, ofisi za Parokia na Kanisa la Kuabudia lenye Groto la Mama Bikira Maria na la Mt. Yosefu. Kazi kubwa ya kamati hii ni kutekeleza uamuzi wa Parokia katika eneo hilo la ujenzi na pia kamati hiyo imekuwa na wajibu wa kutoa ushauri wa namna bora ya kufikia na kutekeleza masuala ya ujenzi
3	Kamati Maalumu	Iliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 2016 ili kuendeleza kazi ya iliyokuwa kamati ya hamasa ambayo ilimaliza kazi ya msingi ya kuelimisha Wanaparokia na pia ilikuwa na jukumu la kusaidia

		uhamasishaji wa michango ya ujenzi wa Kanisa jipya Ni kamati iliyosheheni wasomi, wataalamu na wazoefu wenye karama mbalimbali. Kazi kubwa ilikuwa kufikiria na kuibua mawazo mapya ya maendeleo Parokiani, kuingiza katika mikakati ya utekelezaji mawazo ya Parokia na kuishauri Kamati Tendaji Parokia namna bora ya kufikia malengo ya Parokia. Mwenyekiti wa kwanza wa Kamati hii alitoka kuwa mwenyekiti wa pili wa kamati ya Hamasa ya Parokia na katika uchuguzi uliofanyika mwaka huo alichaguliwa kuwa Katibu wa HWP.
4	Kamati ya Zaka na Mavuno	Iliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 2017 ili kuongeza nguvu ya kuhamasisha Wanaparokia kujitoa zaidi katika kutoa zaka na mavuno Parokiani ili kuongeza makusanyo ya fedha za kuendeleza maendeleo mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa Kanisa kubwa, choo na ofisi ya Parokia Kazi yao kubwa ni kuratibu shughuli za Zaka na Mavuno Parokiani na Jimboni. Aidha, kamati inajihusisha kuendesha semina, hukusanya maoni kutoka kwa

		waamini na kujadili mambo kadha wa kadha na KTP katika kufanikisha utoaji wa Zak ana Mavuno. Moja ya mafanikio ya kamati hii ni mbinu na njia zinazotumika ikiwamo za Bahasha na Zaka kidijiti.
5	Kamati ya Sherehe	Iliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 2019 baada ya kuwapo kwa matukio na sherehe mbalimbali zinazohitaji kuratibiwa na kusimiwa na Wanaparokia kwa umuhimu wake. Baadhi ya shughuli za kamati za kuziratibu na kuzisimamia ni Mkutano Mkuu wa Halmashauri ya Jimbo Kuu la Dar es Salaam uliofanyika Desemba 2019, Sherehe za Komunio ya Kwanza na Kipaimara, sherehe za Uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka 10 ya Parokia na Kutabaruku Kanisa la Parokia. Kimsingi Kamati ya Sherehe imepewa jukumu la kuratibu shughuli za tafrija na sherehe mbalimbali katika ngazi ya Parokia. Kamati hii ni kiungo bora sana kwa Wanaparokia kwani suala la sherehe huwaunganisha Wanaparokia wetu kwa lengo la kukumbuka siku hiyo, kufurahia kwa sala, kula, kunywa na kuburudika.
6	Kamati ya Mabenchi	Iliundwa mwaka 2020 kwa ajili ya kuratibu utengenezaji wa mabenchi ya Kanisa la kudumu. Kazi kubwa ilikuwa

		kusimamia ushauri wa aina ya mabenchi na mwisho utengenezaji wake. Pia, kuhakikisha mabenchi yanatengenezwa na kufikishwa Kanisani kwa muda uliopangwa na kukubalika na Mkandarasi.
7	Kamati ya Ununuzi wa Gari	Iliundwa mwaka 2021 kwa lengo la kuratibu ununuzi wa gari jipya la Parokia. Walihusika kuanzia kuratibu uchangiaji wa fedha za kununulia, kununua na kukamilisha michakato ya usajili na kufikishwa Parokiani na kulikabidhi.

5. **Kujenga imani na uaminifu katika uongozi wa Parokia** – Kwa kuwa kamati zinajumuisha Wanaparokia wenyewe, zimekuwa kiungo muhimu cha kuimarisha imani na ushirikiano kati ya waumini na uongozi wa Parokia.
6. **Kuandaa na Kulea Viongozi wa Baadaye** – Kupitia kamati hizo, wanakamati wanapokea mafunzo na semina kuhusu mipango ya Parokia, hali inayowawezesha kuelewa masuala msingi ya uongozi wa Kanisa. Utaratibu huu unawaandaa kwa majukumu ya uongozi, na kwa njia hiyo, baadhi yao huanza kutambulika na Wanaparokia kama viongozi wenye uwezo na sifa zinazofaa kwa nafasi za uongozi wa Parokia katika siku za usoni.

Kwa utaratibu huu wa ushirikishwaji, uongozi wa Parokia ya Makabe umejenga jamii imara ya waamini wanaoshiriki kikamilifu katika maendeleo ya Parokia na maisha ya kiroho. Mungu aendelee kuwabariki Wanaparokia wa Makabe ili

waendelee kuwa na moyo wa kujitolea kwa maendeleo ya Parokia. Amina.

Umoja na Ushirikiano: Nguzo Kuu ya Maendeleo ya Parokia ya Makabe

Umoja na ushirikiano miongoni mwa Wanaparokia wa Makabe ni msingi imara wa maendeleo yanayoendelea kushuhudiwa. Paroko wa Pili wa Makabe Mh. Pd. Chinnapani Amaladoss aliwahi kusema, *"Mimi nawapenda Wanamakabe kwa kuwa wana ushirikiano mkubwa sana. Kila mmoja anapenda ashiriki suala la maendeleo, hivyo, imekuwa rahisi kwa viongozi kuwafikia na kuwaeleza mpango wa maendeleo na wakaukubali bila matatizo"*. Kauli hiyo imeafikiwa na KTP kwa kusema, "*Mambo mengi Parokiani yamewezekana kutokana na mshikamano mkubwa na matoleo ya hali na mali kutoka kwa waamini wenyewe"*. Vivyo hivyo Paroko wa sasa (wakati kitabu hiki kinaandikwa) Mh. Pd. A. Amalraj katika mikutano na HWP amewahi kusikika akisema, *"Kila wakati najisikia vizuri sana kwa Wanamakabe kwa kuwa kila wakati mnajitoa kushiriki maendeleo ya Parokia yenu. Mimi na Padre mwingine yeyote ni watu wa kupita lakini ninyi hapa ni kwenu. Kwa hiyo, ushirikiano wenu ni kitu muhimu sana kwangu mimi kama Paroko au kwa Padre mwingine yeyote"*.

Katika historia ya makanisa mengi, changamoto kubwa imekuwa ni upungufu wa ushirikiano kati ya viongozi wa Parokia na waamini wao. Katika baadhi ya Parokia, viongozi wanakumbana na ugumu wa kuanzisha na kutekeleza mipango mipya ya maendeleo kutokana na changamoto za uaminifu, ukosefu wa mshikamano, na kutokubalika kwa urahisi.

Hata hivyo, Parokia ya Makabe inajivunia kuwa mfano bora wa mshikamano wa kweli. Ushirikiano wa karibu kati ya viongozi wa Parokia, Halmashauri ya Walei wa Parokia (HWP), na Wanaparokia umesaidia kuhakikisha kuwa kila mpango wa maendeleo unakubaliwa na kutekelezwa kwa mafanikio. Hii imeifanya Makabe kuwa Parokia yenye maendeleo endelevu, hali inayopaswa kuendelezwa na kulindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa kuendelea kudumisha mshikamano huu, Parokia ya Makabe inaweza kufanikisha mambo makubwa zaidi, ikiwemo kuboresha huduma za kiroho, kijamii, na miundombinu ya Kanisa kwa ujumla. Umoja ni nguvu, na pale ambapo panakuwa na mshikamano wa kweli, maendeleo huwa ni jambo lisiloepukika. **Fahari yetu ni mshikamano wetu!**

SURA YA NNE

Maendeleo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Ujenzi wa Kanisa la kwanza, Nyumba ya Mapadre na Ofisi za kwanza za Parokia

Ufahari na bubujiko la shukurani kwa Mungu wetu ni pale tunapoona Maendeleo Parokiani Makabe yaliyoanza kutekelezwa kabla ya kupanda hadhi ya kuwa Parokia kwa kujenga Kanisa la kwanza mwaka 1984, nyumba ya Mapadre kuanzia mwaka 2007 na kukamilisha mwaka 2009 na baadaye kidogo zikajengwa ofisi za kwanza za Parokia. Kwa sasa ofisi hizo za kwanza za Parokia ndio ofisi za Halmashauri ya Walei Parokia (HWP), SACCOS ya Parokia na WAWATA. Majengo hayo yalijengwa kwa nguvu za Wanamakabe ambayo yalisaidia kupanda hadhi ya kuwa Parokia na tunapotafakari hayo tunaishia kusali (Zab. 51:6, 10, 15-19)[7]. Kabla ya ujenzi wowote tulisimuliwa na mmoja wa waamini

[7] Zaburi 51
6 Tazama, wapendezwa na kweli iliyo moyoni; Nawe utanijulisha hekima kwa siri,
10 Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu
15 Ee Bwana, uifumbue midomo yangu, Na kinywa changu kitazinena sifa zako.
16 Maana hupendezwi na dhabihu, au ningeitoa, Wewe huridhii sadaka ya kuteketezwa.
17 Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau.
18 Uitendee mema Sayuni kwa radhi yako, Uzijenge kuta za Yerusalemu.
19 Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za haki, Na sadaka za kuteketezwa, na kafara. Ndipo watakapotoa ng'ombe Juu ya madhabahu yako.

wa mwanzo wa Parokia ya Makabe Mzee wetu Baba Ndele, *"Wanamakabe walikuwa wanasali kwenye kibanda cha useremala cha ndugu Sylvester Edwin Mwale. Kwa kifupi kibanda hicho kilijengwa kwa miti na matope na mwenyewe ndugu Sylvester Edwin Mwale (maarufu kama MY BOY) miaka ya kati au ya mwisho ya 1970".* Baada ya waamini kuzoea kusalia hapo ndugu Sylvester Edwin Mwale au My Boy aliamua kulitoa eneo lake kwa ajili ya Kanisa.

Baada ya kupata eneo hilo kutoka kwa Ndugu Sylvester Edwin Mwale mnamo miaka ya mwanzoni mwa 1980 Wanamakabe wakiongozwa na Shirika la Bikira Maria Consolata (Wakonsolata) waliona ni muhimu kujenga Kanisa la kudumu la kusalia (Picha ya 1). Tulisimuliwa kuwa ujenzi ulifanyika kwa kasi kubwa chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Padre Luciano aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Mt. Paulo Mtume Ubungo Msewe. Wanamakabe waliona fahari sana kuwa sehemu ya kufanikisha ujenzi wa Kanisa hilo kulingana na masimulizi ya Pd. Luciano kuwa, *"Nguvukazi yote ilitoka katika matoleo ya Wanamakabe hii kwa kujitolea kusomba matofali, mchanga, kusaidia mafundi, kuchota maji, kujaza kifusi ndani ya jengo na la kusisimua zaidi ni pale mafundi walipogwaya mbinu ya kushindilia kifusi. Akina mama wa Makabe waliamua kucheza ngoma za Kimakonde juu ya kifusi hadi kikajishindilia vizuri kabisa".* Kanisa hilo la kwanza lilitanuliwa pande zake mbili kati ya mwaka 2006 na 2007 ili kuongeza ukubwa wa eneo la kusalia kulingana na masimulizi ya Bwana Deo Chuwa aliyewahi kuwa kiongozi katika nafasi mbalimbali za Kigango na Parokia.



Picha ya 1: Kanisa la kwanza la Parokia Makabe lililojengwa miaka ya mwanzo ya 1980.

Ujenzi wa Kanisa Kubwa la Kudumu

Baada tu ya kupanda hadhi ya kuwa Parokia mara moja harakati za kuendeleza Parokia zilikuwa ni kujenga kanisa jipya kubwa la Parokia (picha ya 2). Hii ilitokana na kuwa Parokia ilikuwa na Kanisa dogo lililojengwa miaka ya mwanzo ya 1980 ambalo lilikuwa linaweza kuingiza kwa wakati mmoja waamini wachache sana waliokadiriwa kuwa 100 na zaidi kidogo. Kwa hali hiyo, Bwana Deo Chuwa (aliyewahi kuwa Kiongozi wa Kigango na Parokia kwa nafasi mbalimbali) na pia Mzee Paul Luanda (aliyekuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa Parokia ya Makabe) walisema, *"Mahitaji ya kujenga Kanisa kubwa yalikuwa dhahiri na hivyo uamuzi wa kujenga Kanisa kubwa ulifanyika na ujenzi ukaanza rasmi mwaka 2011 na kukamilika mwaka 2020. Ujenzi wa Kanisa hilo uliwashirikisha*

Wanaparokia wote kwa njia tofautitofauti tangu awali hadi kukamilika kwake ikiwamo samani zote za Kanisa".



Picha ya 2: Kanisa la jipya na kubwa la Parokia Makabe lililojengwa Kuanzia 2011 hadi 2020.

Ujenzi wa kanisa kubwa ulikuwa kipaumbele sana kwa Wanaparokia wa Makabe na hivyo walijitoa kwa hali zote. Mfano mzuri wa matoleo ya Wanamakabe ni michango yao ya hali na mali ya fedha, vifaa vya ujenzi na nguvukazi wakati wote wa ujenzi. Aidha, Wataalamu mbalimbali wa ujenzi walijitoa kwa moyo wote kushiriki ujenzi wa kanisa kwa kutoa utaalamu wao bila malipo zaidi ya posho hasa ya usafiri wakiwa wanakwenda kununua mahitaji ya ujenzi na wakati mwingi hata nauli walikuwa wanajitegemea. Kwa namna ya pekee wanakumbukwa wataalamu wafuatao:

i. Msanifu Tresius Ngugo (Parokia ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu – ndiye aliyesanifu mchoro na kusimamia ujenzi wa msingi)
ii. Quantity Surveyor (QS) Patrick Tarimo wa Parokia ya Makabe (Alijitolea kwa hali na mali kufanya kazi ya makadirio ya gharama za kazi za ujenzi na ndiye alikuwa kiongozi wa kamati hiyo)
iii. Hayati Mhandisi Theophil Mfala (Parokia ya Mshikamano, ndiye aliyekuwa Msimamizi Mkuu wa Ujenzi)
iv. Mhandisi Michael Mapunda (Kati ya wasimamizi wa mwanzo wa ujenzi wa kanisa)
v. Msanifu Veran Matunda (Alijitolea sana muda na ujuzi wake kuboresha kazi za usanifu wakati ujenzi ukiendelea)
vi. Mhandisi Charles Mlingi (Alijitoa kwa hali na mali kusimamia kazi hasa baada ya kupauliwa kwa kanisa).
vii. Mhandisi Otieno – Kazi ya umeme
viii. Fundi Wilhelm Haule
ix. Mama Hilda Latela
x. Jackson Kamhabwa
xi. Lowrand Iresa
xii. Hayati Zeno Kisengi
xiii. Kweka
xiv. Hayati Rosemary Misiyani
xv. Gaston Mtei
xvi. Mwl. Keneth
xvii. Mhandisi Remigius Rweyemamu
xviii. Mhandisi Francis Maganga
xix. Adv. Beatrice Mapunda

Ujenzi wa Ofisi Nzuri za Parokia

Maendeleo mengine ya kujivunia na kujisifia ni Ofisi nzuri na ya kisasa ya Parokia iliyojengwa mwaka 2020 sehemu ya chini ya kanisa. Ofisi hiyo mpya ni kubwa na ina jumla ya vyumba vya kutumia saba na ukumbi wa kusubiria ambao unatumika pia kwa vikao mbalimbali vya Parokia. Kufuatana na maelezo ya Halmashauri ya Walei ya Parokia *"Parokia imefanikisha kujenga ofisi inayokidhi mahitaji ya kiofisi ya kichungaji ya Parokia yaliyofikiriwa tangu mwanzo kabisa wa kuanzishwa Parokia. Kuna wakati tuliamua kuzitanua ofisi za mwanzo lakini ilikuwa bado imebana na haikutoa nafasi nzuri ya kutolea huduma za kiroho na kichungaji. Tunamshukuru Mungu kuwa sasa tumefanikiwa kutengeneza ofisi yenye kukidhi mahitaji hayo"*. Ofisi hiyo sasa imetenganisha shughuli za kawaida za Walei kutoka kwenye ofisi za mwanzo na kufanya shughuli za kichungaji zinazohusisha Paroko na wasaidizi wake yaani Paroko Msaidizi na Makatekista kuwa karibu-karibu.

Mandhari na Mazingira ya Parokia ya Makabe

Katika jitihada za kuunda mazingira mazuri na tulivu katika ofisi na kanisa la Parokia ya Makabe, bustani maridadi za maua zimetengenezwa kwa ustadi mkubwa. Maboresho haya yameongeza uzuri wa mandhari ya Parokia, na kufanya eneo lote kuwa la kuvutia na lenye utulivu wa kiroho.

Hatua ya kwanza ya maboresho ilikuwa kusawazisha ardhi, hasa kwa kuzingatia kuwa eneo la kanisa lina mteremko wa asili. Ili kuhakikisha matumizi bora ya eneo hilo, sehemu za chini zilifanyiwa marekebisho na kuunganishwa kwa njia za kupita kwa urahisi. Lango kuu la uzio wa kanisa limeboreshwa kwa mpangilio mzuri, huku ngazi mbili zikijengwa kwa

ubavuni mwa kila upande wa kanisa ili kurahisisha upatikanaji wa ofisi ya Parokia iliyoko chini ya eneo la kanisa.

Aidha, ngazi maalum zimeundwa ili kufanikisha kufika mlango mkuu wa kanisa kwa urahisi. Hili lilikuwa suluhisho la changamoto ya kijiografia ya eneo, kwani lilisaidia kuleta mwonekano wa kupendeza na kuongeza thamani ya matumizi ya eneo la Parokia. Maboresho haya yameifanya Parokia ya Makabe kuwa mfano wa utunzaji wa mazingira ya kiimani, yakichangia kuleta utulivu kwa waamini wanaokuja kusali na kutekeleza shughuli mbalimbali za Parokia.

Kwa mujibu wa maoni ya Wanaparokia Bwana Dominic Ndoliki Ntapala na Bwana Gasper Tluway, maboresho haya yameifanya Parokia kupendeza zaidi na kuwa mahali bora pa ibada na mikusanyiko ya kiroho. Mazingira safi na yaliyopangwa kwa umakini yanachangia si tu mandhari nzuri, bali pia kuinua hali ya kiroho kwa wanaparokia wa Parokia ya Makabe.

Maendeleo ya huduma za Imani katika Parokia Bikira Maria Consolata Makabe

Moja ya mafanikio makubwa ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe ni kuimarika kwa huduma zinazokoleza imani miongoni mwa waumini. Tangu kuanzishwa kwake, Parokia ilikuwa na vyama vya kitume vichache, ambapo vilivyojulikana zaidi ni WAWATA, UWAKA, VIWAWA, Shirika la Mt. Vincent wa Paulo, na UKWAKATA.

Hata hivyo, Parokia iliweka mkakati wa kukuza na kuimarisha vyama vya kitume, na kufikia mwaka 2022, imefanikiwa

kuongeza idadi ya vyama hivyo na kuhakikisha vinafanya kazi ya utume kwa ufanisi zaidi. Vifuatavyo ndio vyama vilivyopo Parokiani Makabe Machi 2025: WAWATA, UWAKA, VIWAWA, UKWAKATA, Karizmatiki Katoliki, Legio Maria, Mt. Anna, Mt. Vincent wa Paulo, Moyo Mtakatifu wa Yesu, Utoto Mtakatifu, CPT, Chama cha Wazee na Wastaafu cha Mtakatifu Agustino, Watumishi wa Altare, Mama Anna, na Rozari Hai.

Vyama hivi vimekuwa vikikua na kuimarika na kuwa chachu kubwa ya maendeleo ya kiroho na kijamii kwa waamini wa Parokia. Kwa mfano, UKWAKATA kilianza na kwaya moja lakini sasa Machi 2025 kimekua na kuwa na kwaya tatu, huku ya kwaya ya nne ya Watoto ikiwa katika hatua za kuijenga.

Kazi za Vyama vya Kitume katika Kanisa Katoliki
Vyama vya kitume katika Parokia ya Makabe vina jukumu muhimu katika kukuza imani, mshikamano, na maendeleo ya kiroho na kijamii miongoni mwa wanaparokia. Kupitia shughuli mbalimbali, vyama hivi vinasaidia kuimarisha maisha ya kiroho ya waumini kwa kuandaa na kushiriki ibada kama Rozari, Novena, na Sala za pamoja kwa ajili ya wanaparokia na taifa la Mungu. Pia, vyama hivi vina jukumu la kuratibu mafungo na semina za kiroho kwa wanachama na waamini wengine, ili kuwasaidia kuelewa na kuishi imani yao kwa kina zaidi.

Mbali na huduma za kiroho, vyama vya kitume katika Parokia ya Makabe vinatekeleza majukumu ya kijamii kwa kuwasaidia wahitaji kama wagonjwa, wazee, na yatima, wakidhihirisha upendo wa Kikristo kwa matendo. Kwa mfano, kupitia Shirika la Mtakatifu Vicent wa Paulo, vyama hivi vimekuwa vikitoa

misaada ya chakula kwa wahitaji mbalimbali kila mwezi. Aidha, vyama hivi vinawapa faraja na msaada wa kifedha na kihisia wale wanaokumbwa na changamoto kama vifo, majanga, na magonjwa, kuhakikisha hakuna anayebaki peke yake katika nyakati ngumu.

Katika kuimarisha mshikamano wa Kikristo, vyama vya kitume vimekuwa chachu ya kuhamasisha upendo na mshikamano miongoni mwa wanaparokia. Mojawapo ya njia za kufanikisha hili ni kupitia utoaji wa elimu katika ngazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na JNNK na kanda. Aidha, vyama hivi vinashiriki kikamilifu katika maendeleo ya Parokia, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa makanisa, ofisi, na nyumba ya mapadre, kuhakikisha kuwa miundombinu ya Kanisa inaboreshwa kwa ajili ya ukuaji wa imani na huduma kwa waumini.

Kwa ujumla, vyama vya kitume ni nguzo muhimu katika ukuaji wa Kanisa Katoliki, vikichangia si tu katika maendeleo ya kiroho bali pia ya kijamii kwa waumini wote. Kupitia huduma zao, wanajenga jamii yenye mshikamano, inayosaidiana, na inayoishi mafundisho ya Kristo kwa vitendo. Ushiriki wao katika shughuli za Kanisa umeleta maendeleo makubwa katika Parokia na jamii kwa ujumla, kwa kuhakikisha kuwa imani inadhihirishwa kwa matendo ya upendo na mshikamano.



Picha: Kamati Tendaji ya UWAKA 2022. Kutoka kushoto ni Eng. Remigius Rweyemamu (Katibu Msaidizi; Ndugu Charles Sangawe (Makamu Mwenyekiti); Ndugu Osward Mramba (Mwenyekiti); Ndugu Alex Ally (Katibu), Ndugu Ambrose Mpili (Mhazini Msaidizi); na Ndugu Efrem Massawe (Mhazini).

Kuongeza maeneo ya Parokia ya Bikira Maria Consolata Makabe

Kwa ajili ya maendeleo na hasa ufanisi mkubwa wa kutoa huduma za kiroho na kimwili, Parokia iliamua kuongeza eneo la Parokia iliyopo. Parokia iliamua kuongea na wenyeji ambao ni majirani ili waweze kuwauzia maeneo hayo. Kwa moyo wao wa upendo walikubali na mwaka 2014 Parokia ikanunua maeneo hayo na kuongeza ukubwa wa eneo la Kanisa. Eneo lililonunuliwa lilikuwa na majengo mawili, moja ikiwa ni

nyumba yenye mwonekano wa kighorofa na lingine ni jengo dogo la kuendeshea biashara maarufu kama fremu za maduka.

Aidha Parokia ilinunua eneo lingine mpakani na Parokia ya Msumi maarufu kwa jina la Kavimbirwa. Eneo hilo kwa sasa baada ya kugawa Parokia na kuanzisha Parokia ya Msumi lipo upande wa Msumi. Hata hivyo, Parokia ya Makabe bado ina mpango wa kanzisha vituo vya sala katika eneo la mpakani na Parokia ya Msumi na pia katika eneo la kituo cha Child in the Sun. Wakati kitabu hiki kinaandikwa mikakati ya kuhakikisha kuwa eneo hilo linapatikana ilikuwa inaendelea ili kutimiza mpango huo wa kuanzisha kituo cha sala.

Parokia pia ina eneo lingine lililopo upande wa pili wa Kanisa. Parokia imepata eneo hilo linalofikia ekari 10 kwa kupewa na Jimbo mwaka 2018. Eneo hilo linafikiriwa kujengwa hospitali kubwa ambayo itamilikiwa na Parokia ya Makabe. Hospitali hiyo imelenga kuwa ya aina yake kwa Jimbo Kuu la Dar es Salaam na kwa taifa ambayo itakidhi hadhi ya kuwa Hospitali ya Jimbo Kuu la Dar es Salaam linalowakilisha taswira ya Kanisa Katoliki Tanzania. Imepangwa kuwa na huduma za kipekee na maalumu kwa Maaskofu, Mapadre, Wanafunzi wa Upadre, Watawa wa kike na wa kiume, viongozi wa Kitaifa na kwa wakazi wa Makabe. Pia, itakuwa na chuo cha uuguzi. Mchakato uliopo sasa ni kwamba Parokia imeunda kamati ya kuratibu mpango huo. Kamati kwa sasa inaendelea na kazi na imeshafanya vikao kadhaa na uongozi wa Parokia na inaelezwa mpango mzima wa mradi huo wa kujenga hospitali kubwa umeshawasilishwa kwa uongozi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam ambao wameupenda na kusema kuwa mipango ya awali iendelee wakati Jimbo likipitia makabrasha

yaliyowasilishwa kwao kuhusiana na mradi huo. Uongozi wa Jimbo ukiupitisha mradi huo, basi utekelezaji wake utaanza mara moja ili kufikia malengo yanayofikiriwa.

Uwezo wa Parokia kujitegemea

Moja ya mambo makubwa sana kwa Kanisa hivi sasa ni kujitegemea lenyewe na kupewa msaada mdogo hasa wa mawazo na mipango. Hilo limekuwa jambo muhimu na la kipaumbele kwa Parokia ya Makabe tangu awali kabisa. Viongozi kwa maana ya Maparoko na Viongozi wa HWP wote wamekuwa katika mtazamo wa kuhakikisha Parokia ya Makabe inajitegemea kikamilifu. Mungu ni mwema katika nia hiyo na Parokia imejijenga na sasa ina uwezo wa kutosha wa kujitegemea. Parokia ina uwezo wa kukusanya mapato yake kutoka vyanzo vilivyo ndani ya uwezo wake na kila wakati imekuwa ikifikia malengo ya mipango inayopangwa. Mfano mzuri ni ujenzi wa Kanisa Kubwa na la kudumu ambao umefanikishwa kwa kutumia Wanaparokia wenyewe kulijenga kwa michango yao tangu mwanzo hadi mwisho.

Kwa kifupi, inatathminiwa kuwa kujitegemea kwa Parokia ya Makabe ni kwa msaada wa Mungu. Parokia hii ya Makabe itaendelea zaidi kimaendeleo kadiri siku na miaka inavyokwenda mbele. Parokia imeongeza uwezo wa kuchangia mapato kwa njia za sadaka, zaka, mavuno na matoleo binafsi na shukurani kwa Mungu. Vyanzo hivyo vimefanikisha wastani wa makusanyo kuwa zaidi ya shilingi za Kitanzania milioni 600 kwa mwaka na hivyo kusaidia uwezo wa kujitegemea. Aidha, Parokia imefanikiwa kuwa na hifadhi ya rasilimali za maendeleo kama vile ardhi, magari, SACCOS kwa ajili ya huduma za fedha na shule ya awali na msingi huku

kukiwa na mpango maridhawa wa kuwa na hospitali kubwa ya Parokia. Hayo yote yanalenga katika kukuza uwezo wa kujitegemea na pia kumpunguzia Mwanamakabe mzigo wa michango mingi. Tunawashukuru Mapadre kwa kuliona hilo kwani fahari yetu Wanamakabe ni kuona Parokia yetu ikiwa na vyanzo imara vya mapato ili kutoa huduma nyingi za kijamii kama vile kusaidia wahitaji, kusomesha waseminari, kuongeza mtaji wa SACCOS ili kukopesha kwa riba ndogo zaidi, n.k.